**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents | Budget Guidelines

2021

# Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022

Tanzania, United Republic

Ministry of Finance and Planning

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/216

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22

**Februari, 2021**

YALIYOMO

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ iii

**MUHTASARI** ........ v

**SEHEMU YA KWANZA** ........ ix
**SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI** ........ ix

**SURA YA KWANZA** ........ 1
**MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI** ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda ........ 1
1.3 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei ........ 3
1.4 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania ........ 3
1.5 Deni la Serikali ........ 8
1.6 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Tanzania ........ 9

**SURA YA PILI** ........ 11
**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2019/20** ........ 11
2.1 Utangulizi ........ 11
2.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/20 ........ 11
2.2.1 Mapato na Matumizi ........ 11
2.2.1.1 Mapato ya Ndani ........ 11
2.2.1.2 Misaada ........ 12
2.2.1.3 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti ........ 12
2.2.1.4 Matumizi ........ 13
2.2.2 Utekelezaji wa Bajeti Katika Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21 ........ 13
2.2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ........ 14
2.2.4 Mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati ........ 15
2.2.4 Mafanikio Mengine Yaliyopatikana ........ 26
2.2.5 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti ........ 29
2.2.6 Hatua Zinazochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti ........ 29

**SURA YA TATU** ........ 31
**MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22** ........ 31
3.1 Utangulizi ........ 31
3.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla ........ 31
3.3 Misingi ya Uchumi Jumla (Assumptions) ........ 31
3.4 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati ........ 31
3.5 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati ........ 34
3.6 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati ........ 39

3.7 Mkakati wa Kugharamia Nakisi ya Bajeti ... 40
3.8 Vipaumbele katika Muda wa Kati ... 41
3.9 Makadirio ya Bajeti ... 43

**SURA YA NNE ... 49**
**USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA BAJETI ... 49**
4.1. Utangulizi ... 49
4.2. Vihatarishi vya Uchumi na Bajeti ... 49
4.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi ... 51

**SEHEMU YA PILI ... 53**
**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22 ... 53**

**SURA YA KWANZA ... 54**
**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22 ... 54**
1.1. Uandaaji wa Mpango na Bajeti ... 54
1.1.1. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ... 54
1.1.2. Kamati za Bajeti ... 55
1.1.3. Maandalizi ya Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 55
1.1.4. Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara ... 55
1.2. Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti ... 56
1.3. Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ... 62
1.4. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 63
1.4.1. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa ... 63
1.4.2. Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 64
1.5. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep ... 68
1.6. Uchambuzi wa Mpango na Bajeti ... 68
1.7. Uwasilishaji wa Randama ... 69
1.8. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji ... 69
1.8.1. Ufuatiliaji na Tathmini ... 69
1.8.2. Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji ... 69

**MUUNDO WA UWASILISHAJI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22 ... 71**
2.1. Utangulizi ... 71
2.2. Maandalizi ya Mpango na Bajeti ... 71
2.3. Utekelezaji wa Bajeti ... 72
2.4. Taarifa za Utekelezaji ... 72

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGITF | Agricultural Inputs Trust Fund |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited |
| BRELA | Business Registration and Licensing Agency |
| CBMS | Centralized Budget Management System |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CFR | Council Financial Report |
| CFS | Consolidated Fund Service |
| COVID - 19 | Coronavirus Disease |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| DAWASA | Dar es Salaam Water and Sewage Authority |
| DCF | Development Co-operation Framework |
| DEV | Development |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| EAC | East African Community |
| EFD | Electronic Fiscal Device |
| EFDMS | Electronic Fiscal Device Management System |
| EPZ | Export Processing Zone |
| FFARS | Facility Financial Accounting and Reporting System |
| FY | Financial Year |
| FYDP | Five Year Development Plan |
| GAMIS | Government Asset Management Information System |
| GAMS | Government Arrears Management System |
| GBS | General Budget Support |
| GCLA | Government Chemist Laboratory Authority |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| GFS | Government Finance Statistics |
| GNI | Gross National Income |
| GPD | General Purpose Grant |
| GPSA | Government Procurement Service Agency |
| HCMIS | Human Capital Management Information System |
| iCHF | Community Health Fund |
| ICT | Information Communication Technology |
| IMF | International Monetary Fund |
| LGAs | Local Government Authorities |
| LGRCIS | Local Government Revenue Collection Information System |
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| M3 | Extended Broad Money Supply |
| MDAs | Ministries, Independent Departments and Agencies |
| MTEF | Medium Term Expenditure Framework |
| MTSPBM | Medium Term Strategic Plan and Budget Manual |

| | |
|---|---|
| MUSE | Mfumo wa Uhasibu Serikalini |
| MW | Megawatts |
| NACSAP | National Anti - Corruption Strategy and Action Plan |
| NFRA | National Food Reserve Agency |
| NHIF | National Health Insurance Fund |
| NPMIS | National Project Management Information System |
| OC | Other Charges |
| OTRMIS | Office of Treasure Registrar Management Information System |
| PE | Personal Emoluments |
| PIM - OM | Public Investment Management – Operational Manual |
| PlanRep | Planning and Reporting Database |
| POS | Point of Sale |
| PPP | Public-Private-Partnership |
| PSRP | Public Sector Reform Program |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| RSs | Regional Secretariats |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SDG | Sustainable Development Goals |
| SEZ | Special Economic Zone |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| SOPS | Standard Operating Procedures |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANePS | Tanzania National e-Procurement System |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| TBA | Tanzania Buliding Agency |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMESA | Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency |
| TeSWs | Tanzania Electronic Single Window System |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs Authority |
| TIB | Tanzania Investment Bank |
| TIC | Tanzania Investment Centre |
| TIKA | Tiba Kwa Kadi |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TSA | Treasury Single Account |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VAT | Value Added Tax |
| VVU | Virusi Vya Ukimwi |
| WAVIU | Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |
| WCF | Workers Compensation Fund |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |

# MUHTASARI

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 unatoa maelekezo ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti. Mwongozo wa mwaka 2021/22 umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439.

Katika uandaaji wa Mwongozo huu, uchambuzi wa nyaraka mbalimbali ulifanyika kwa lengo la kuainisha sera, vipaumbele na maelekezo ya Serikali yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wa uandaaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2021/22. Nyaraka hizo ni pamoja na: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26; na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada, Sura 134; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Agenda ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeyaridhia.

Mwongozo umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza ni Sera na Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 ambayo ina Sura nne (4). Sura ya Kwanza inahusu Mapitio ya Mwenendo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, ambapo inaelezea mapitio ya mwenendo wa hali ya uchumi nchini, kikanda na dunia kwa mwaka 2019/20, na mwelekeo katika mwaka 2020/21. Sura ya Pili ni Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/20 ambayo imebainisha mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza na hatua za kukabiliana na changamoto husika. Sura ya Tatu ni Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22, ambapo imeainisha sera za kibajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2021/22 na katika muda wa kati. Sura ya Nne inahusu Usimamizi wa Vihatarishi vya Bajeti kwa mwaka 2021/22 ambapo imebainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti na hatua za kukabiliana na vihatarishi husika. Aidha, Sehemu ya Pili ya Mwongozo ni maelekezo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22.

Mapitio ya mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2019 yameonesha kuwa uchumi wa Tanzania uliendelea kuimarika ambapo Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.0 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Sekta zilizochangia zaidi katika ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2019 ni pamoja na ujenzi (asilimia 24.9), kilimo (asilimia 20.2), viwanda (asilimia 9.6), usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.3) na biashara (asilimia 7.3). Aidha, kwa mwaka 2020, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.5. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zinazotarajia kuwa na ukuaji chanya mwaka 2020 kutokana na hatua za Serikali za kutowafungia watu ndani na kuwaruhusu waendelee na shughuli za kiuchumi. Vile vile, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua na kufikia wastani wa asilimia 6.3 katika muda wa kati.

Katika mwaka 2019/20, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 20,290.2, sawa na asilimia 88.0 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 17,622.8 zilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, sawa na asilimia 92.3 ya lengo. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 717.2, sawa na asilimia 93.7 ya lengo. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilipokea misaada ya shilingi bilioni 927.8 sawa na asilimia 76.8 ya lengo. Mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi bilioni 2,588.2, sawa na asilimia 164.3 ya lengo. Vile vile, Serikali ilikopa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara ya shilingi bilioni 1,822.1, sawa na asilimia 78.7 ya makisio.

Kwa upande wa matumizi, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 28,573.1 katika mwaka 2019/20, sawa na asilimia 86.3 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 20,208.0 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 96.9 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8,365.10 ni fedha za maendeleo zilizopitia Mfuko Mkuu wa Serikali, sawa na asilimia 68.3 ya bajeti ya maendeleo.

Katika mwaka 2021/22, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 26,032.6 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 24,065.5 mwaka 2020/21. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 8.6 hadi shilingi bilioni 30,852.1 mwaka 2023/24. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 71.7 mwaka 2021/22 hadi asilimia 76.7 mwaka 2023/24. Katika kipindi hicho, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 36,258.8, sawa na asilimia 22.1 ya Pato la Taifa, kutoka makadirio ya shilingi bilioni 34,879.8 mwaka 2020/21. Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 4.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 40,207.4 mwaka 2023/24.

Vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka 2021/22 ni pamoja na: ukamilishaji wa miradi ya kimkakati ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ikiwemo: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge); Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga; Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222); Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu (Interchange) wa Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na ununuzi wa Meli za Uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay Kaskazini; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii; na uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi.

Maeneo mengine ya vipaumbele ni: kuongeza uzalishaji viwandani kwa kuwezesha upatikanaji wa malighafi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, bidhaa za plastiki, *aluminium*, mbegu za mafuta (alizeti, chikichi, ufuta), uzalishaji wa sukari, ngozi na nguo; kufanya tafiti za kina kwa ajili ya maendeleo ya viwanda; kuongeza uwekezaji katika ujuzi, usafirishaji na nishati; kuanzisha vituo vya biashara na huduma (logistic centres) katika maeneo muhimu ya uzalishaji na usafirishaji nje; kuendeleza ujuzi ikiwemo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya; kuimarisha mfumo wa Bima ya Afya; kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa; kuimarisha utafiti wa tiba asili na tiba mbadala; afya na ustawi wa jamii; kinga ya jamii; usalama wa chakula na lishe; kuboresha sekta ya maji; mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi; na utawala bora na utawala wa sheria.

Katika kufanikisha vipaumbele hivyo, Mwongozo umeainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa. Baadhi ya maelekezo hayo ni pamoja na: kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Mafungu; kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia muundo wa Matumizi

wa Muda wa Kati (Medium Term Expenditure Framework - MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi; kuzingatia viwango vya ukomo wa bajeti vitakavyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango; kujumuisha gharama za miradi inayoendelea katika bajeti kabla ya kuanzisha miradi mipya; kufanya ukadiriaji sahihi wa matumizi yasiyoepukika husussan stahili za kisheria za kiutumishi, gharama za pango, umeme, simu, maji, ulinzi na usafi; kutenga fedha za kulipa madeni yaliyohakikiwa; kuandaa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Katibu Mkuu UTUMISHI; kuandaa mpango kazi na mpango wa mahitaji ya fedha kwa wakati; kuhakikisha Kamati za Bajeti za Mafungu zinafanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake; na kuandaa taarifa za utekelezaji kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Mwongozo.

# SEHEMU YA KWANZA

# SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI

# SURA YA KWANZA

## MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

### 1.1 Utangulizi

1. Sura hii inawasilisha mapitio ya mwenendo wa hali ya uchumi nchini, kikanda na dunia kwa mwaka 2019/20, na mwelekeo katika mwaka 2020/21. Mapitio ya hali ya uchumi nchini yanazingatia Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/20 na robo ya kwanza ya mwaka 2020/21, ambayo ililenga kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20, Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Agenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Vipaumbele hivyo vilihusisha: Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Maendeleo ya Watu; Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; na Kuimarisha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango.

### 1.2 Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Sehemu hii inaelezea mwenendo wa uchumi wa dunia na kikanda kwa mwaka 2019/20, mwelekeo wake kwa mwaka 2020/21, na athari zake katika uchumi nchini.

#### 1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Mwelekeo Wake

3. Katika mwaka 2019, uchumi wa dunia ulikuwa imara, japokuwa ulikua kwa kasi ndogo ya asilimia 2.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Kasi ndogo ya ukuaji ilichangiwa na kuendelea kwa mgogoro wa kibiashara kati ya China na Marekani, kuongezeka kwa machafuko ya kijamii katika baadhi ya nchi, pamoja na majanga yanayohusiana na hali ya hewa, ikiwemo vimbunga, ukame na mafuriko katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilichangia kupunguza uwekezaji na biashara duniani. Kulingana na taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Oktoba 2020, uchumi wa dunia unatarajiwa kuporomoka hadi kufikia ukuaji hasi wa asilimia 4.4 mwaka 2020 kutokana na athari za ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu (*COVID-19*). Hata hivyo, uchumi wa dunia unatarajiwa kuongezeka kufikia asillimia 5.2 mwaka 2021, kutokana na matarajio ya kupungua kwa athari za *COVID-19* ambapo uwekezaji na matumizi binafsi vinatarajiwa kuongezeka.

### 1.2.2 Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Mwelekeo Wake

4. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2019 kutoka asilimia 3.3 mwaka 2018. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kumetokana na kupungua kwa shughuli za kibiashara baina ya nchi washirika, mafuriko maeneo ya Mashariki mwa Afrika, ukame maeneo ya Kusini mwa Afrika na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma duniani. Matarajio ni ukuaji hasi wa asilimia 3.0 mwaka 2020 kutokana na athari za *COVID-19* na kuimarika kwa kasi ya ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2021.

### 1.2.3 Ukuaji wa Uchumi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)

5. Uchumi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ulikua kwa wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.9 mwaka 2018. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa bei za bidhaa zinazouzwa na nchi hizo katika soko la Dunia na mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa katika nchi za kusini mwa Afrika. Baadhi ya nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Madagascar, Malawi, Mauritius, Seychelles na Tanzania zilikuwa na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2019. Tanzania ndiyo nchi pekee iliyofikia lengo la Jumuiya la kuwa na kiwango cha ukuaji wa uchumi kisichopungua asilimia 7.0. Kutokana na athari za *COVID-19*, uchumi wa nchi za SADC unatarajiwa kuwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020.

### 1.2.4 Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

6. Mwenendo wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliendelea kuimarika. Uchumi wa nchi hizi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2018. Ukuaji huu ulitokana na uwekezaji katika miradi mikubwa ya miundombinu, kuongezeka kwa matumizi hususan katika sekta za huduma, kuongezeka kwa uzalishaji wa kilimo na kuimarika kwa soko la pamoja na umoja wa forodha wa Jumuiya. Ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2019 kwa nchi hizo za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo: Sudan Kusini asilimia hasi 0.9, Burundi asilimia 1.8, Uganda asilimia 6.7, Kenya asilimia 5.4, Tanzania asilimia 7.0 na Rwanda asilimia 9.4.

**Jedwali Na. 1.1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Maoteo (Asilimia)**

| | Halisi | | Maoteo | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
| Dunia | 3.5 | 2.8 | -4.9 | 5.2 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.2 | 1.7 | -5.8 | 3.9 |
| Nchi Zinazoendelea na Kuibuka | 4.5 | 3.7 | -3.3 | 6.0 |
| China | 6.7 | 6.1 | 1.9 | 8.2 |
| India | 6.1 | 4.2 | -10.3 | 8.8 |
| Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.3 | 3.2 | -3.0 | 3.1 |
| SADC | 2.9 | 2.0 | -3.1 | - |
| EAC | 4.6 | 5.2 | 1.5 | 3.7 |

***Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa, Oktoba, 2020*

## 1.3 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

7. Mfumuko wa bei wa dunia uliendelea kubaki katika kiwango cha chini cha asilimia 3.6 mwaka 2019, kama ilivyokuwa mwaka 2018. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 8.4 mwaka 2019, ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na upungufu wa mazao ya chakula katika masoko kutokana na uwepo wa mafuriko katika baadhi ya maeneo ya mashariki mwa Afrika hususan Tanzania na Kenya yaliyoharibu miundombinu ya usafirishaji. Vile vile, ongezeko hilo lilichangiwa na ukame uliotokea katika baadhi ya maeneo kusini mwa Afrika zikiwemo nchi za Zambia na Zimbabwe.

8. Katika mwaka unaoishia Juni 2020, wastani wa mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifikia asilimia 4.5 kutoka asilimia 2.8 mwaka unaoishia Juni 2019. Katika nchi ya Uganda, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.0, ikilinganishwa na asilimia 3.1 Juni 2019. Nchini Kenya, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 5.5, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.2 Juni 2019. Viwango hivyo vilikuwa ndani ya lengo la Jumuiya, ambapo nchi wanachama zinatakiwa kuwa na mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8.0.

## 1.4 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

9. Mwaka 2018 na 2019, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0. Sekta zilizochangia zaidi katika ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2019 ni pamoja na ujenzi (asilimia 24.9), kilimo (asilimia 20.2), viwanda (asilimia 9.6), usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.3) na biashara (asilimia 7.3). Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na: madini (asilimia 17.7); ujenzi (asilimia 14.8); sanaa na burudani (asilimia 11.2); na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 8.7).

10. Pamoja na mlipuko wa *COVID-19*, mwenendo wa uchumi uliendelea kuwa imara, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani kutokana na maono na ujasiri wa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuruhusu shughuli za kiuchumi na kijamii kuendelea wakati wa mlipuko huo. Vilevile, Tanzania ilipata unafuu kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

11. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2020 (Januari–Machi), uchumi ulikua kwa asilimia 5.7. Sekta zilizokua kwa kasi zaidi ni pamoja na uchimbaji madini (asilimia 15.3); shughuli za utoaji huduma za afya na ustawi wa jamii (asilimia 10.2); na shughuli za kiufundi, kitaalam, na kisayansi (asilimia 8.9).

### 1.4.1 Tanzania Kuwa Nchi Yenye Hadhi ya Uchumi wa Kati wa Chini

12. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9 (2016-2019) imewezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini (lower-middle income) kutoka kundi la nchi za kipato cha chini (low income). Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwezi Julai 2020, wastani wa pato la mtu mmoja mmoja (GNI per capita) uliongezeka kutoka shilingi 1,990,462 (sawa na dola za Marekani 980) mwaka 2015 hadi shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,080) mwaka 2019, hivyo kuvuka kigezo cha dola za Marekani 1,036 cha kuingia katika kundi la nchi za kipato cha kati cha chini. Aidha, utegemezi wa kibajeti umepungua kutoka asilimia 14.0 ya bajeti halisi mwaka 2014/15 hadi asilimia 9.3 mwaka 2019/20.

13. Mafanikio haya yameifanya Tanzania kufikia lengo la kuwa nchi ya kipato cha kati cha chini mapema zaidi ikilinganishwa na matarajio yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Aidha, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 23 za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini. Katika nchi 16 za SADC, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizo na uchumi wa kipato cha kati cha chini. Tanzania na Kenya ndiyo nchi pekee zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini katika nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

14. Mafanikio haya yanatokana na usimamizi na utekelezaji madhubuti wa sera na mipango ya maendeleo na kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji huduma kwa wananchi kama vile elimu, afya, maji, umeme na miundombinu. Maboresho yaliyofanyika katika huduma hizi yamepunguza umasikini na kuboresha maisha ya wananchi, mathalani umaskini wa mahitaji muhimu umepungua toka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18.

15. Umaskini usio wa kipato umekuwa na mabadiliko chanya kama ifuatavyo: idadi ya watanzania wenye bima ya afya imeongezeka kutoka asilimia 27 mwaka 2016/17 hadi asilimia 34 mwaka 2018/19; idadi ya vifo wakati wa kujifungua imepungua kutoka 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi 321 mwaka 2019/20; vifo vya watoto chini ya miaka mitano imepungua hadi 50 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20 kutoka vifo 67 mwaka 2014/15; vifo vya watoto wachanga vimepungua hadi 36 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20 kutoka vifo 43 mwaka 2015/16; kiwango cha ufaulu mitihani ya darasa la saba pamoja na sekondari (Kidato cha nne) kimeongezeka kutoka asilimia 67 na asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 na asilimia 80.7 mwaka 2019 mtawalia; Idadi ya wanufaika wa mkopo wa elimu ya juu imeongezeka kutoka wanufaika 125,126 mwaka 2015 hadi 145,000 mwaka 2020; hali ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini imeongezeka kufikia asilimia 84 na asilimia 70.1 mwaka 2019 kutoka asilimia 74 na asilimia 47 mwaka 2015 mtawalia; Idadi ya kaya zilizounganishwa na umeme imeongezeka kwa asilimia 18.9 huku ongezeko kubwa likiwa maeneo ya vijijini (asilimia 45) ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 12.1 maeneo ya mijini.

### 1.4.2 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

16. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0. Katika mwaka ulioishia mwezi Juni 2020, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Mfumuko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 3.2 Desemba 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.8 Desemba 2019. Hali hii ilichangiwa na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti, uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme, kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na utulivu wa viwango vya kubadilisha sarafu ya Tanzania dhidi ya fedha za nchi nyingine.

17. Mfumuko wa bei za vyakula uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.0 katika mwaka unaoishia Desemba 2020, ikilinganishwa na asilimia 6.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za vyakula kwenye baadhi ya masoko nchini na upungufu wa vyakula kwa nchi jirani na hivyo kuvutia wafanyabiashara nchini kuuza katika masoko hayo yenye upungufu. Aidha, mafuriko yaliharibu miundombinu na kusababisha ongezeko la gharama za usafirishaji wa vyakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada kwenda maeneo yenye upungufu. Vile vile, mafuriko yaliharibu mazao yaliyokuwa shambani na hivyo kupunguza uzalishaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya maeneo nchini. Hata

hivyo, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati ulifikia wastani wa asilimia 2.3 mwaka ulioishia Desemba 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka ulioishia Desemba 2019. Mwenendo huu umechangia kuimarisha uwezo wa wananchi kumudu gharama za maisha, kuchochea shughuli mbalimbali za uwekezaji na uzalishaji, na kuongeza ushindani wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

### 1.4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo

18. Serikali iliendelea kusimamia Sera ya Fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei ili uendelee kuwa tulivu na ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0. Aidha, sera hiyo ililenga kuongeza ukwasi katika sekta ya benki ili kuwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya kukuza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kufuatia usimamizi huo, katika mwaka ulioishia Juni 2020, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 10.0 sawa na lengo la mwaka 2019/20. Hata hivyo, kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2020, ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa wastani wa asilimia 7.4. Aidha, katika kipindi cha mwaka ulioishia Novemba 2020, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 5.2. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mikopo katika uchumi.

19. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 5.2 katika mwaka ulioishia Novemba 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji katika uchumi pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara nchini. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 33.6 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za biashara (asilimia 15.7), uzalishaji viwandani (asilimia 9.9) na Usafirishaji na Mawasiliano (asilimia 8.7).

### 1.4.4 Mwenendo wa Viwango vya Riba

20. Riba za mikopo ziliendelea kupungua kutokana na Sera ya Fedha iliyolenga kuongeza ukwasi na usimamizi wa hatua mbalimbali za kupunguza riba na mikopo chechefu, ikiwamo matumizi ya kanzidata ya taarifa ya historia za wakopaji. Kwa ujumla, riba za mikopo zimepungua kufikia wastani wa asilimia 16.51 katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2020, kutoka asilimia 16.87 Juni 2019 na riba za amana kwa ujumla zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.74 kutoka asilimia 7.44 kwa kipindi hicho cha marejeo.

21. Kati ya Julai hadi Novemba 2020, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na benki ilipungua kufikia asilimia 16.53 kutoka asilimia 16.87 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kwa kipindi kilichoishia Novemba 2020, riba za mikopo zimepungua

kufikia wastani wa asilimia 16.61 kutoka asilimia 16.94 Novemba 2019. Aidha, riba za mikopo za mwaka mmoja zilipungua kufikia asilimia 15.70 Novemba 2020, kutoka asilimia 16.90 Novemba 2019. Vile vile katika kipindi hicho, wastani wa Riba ya Amana ilikuwa asilimia 6.50 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.22 katika kipindi kama hicho 2019. Riba za amana kwa ujumla zilipungua na kufikia asilimia 6.74 Novemba 2020, kutoka asilimia 6.97 Novemba 2019. Kadhalika, riba za amana za miezi 12 zilipungua na kufikia asilimia 8.43 Novemba 2020, kutoka asilimia 9.38 Novemba 2019. Kufuatia mwenendo huo, tofauti ya viwango vya riba ya kukopa ya amana ya mwaka mmoja ilipungua na kufikia asilimia 7.27 kutoka asilimia 7.51 Novemba 2019.

#### 1.4.5 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

22. Katika mwaka 2019/20 thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni iliendelea kuwa tulivu. Kwa mwaka 2019/20, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,289.1 ikilinganishwa na shilingi 2,282.3 mwaka 2018/19. Hii inamaanisha kuwa thamani ya shilingi ilipungua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 0.30 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na asilimia 1.73 mwaka 2018/19. Aidha, katika kipindi cha Novemba 2020, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,297.7 ikilinganishwa na shilingi 2,288.3 Novemba 2019. Hali hii inatokana na usimamizi thabiti wa Sera za Fedha na bajeti.

#### 1.4.6 Mwenendo wa Sekta ya Benki

23. Sekta ya benki imeendelea kuimarika ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya wenye amana na wakopaji. Novemba 2020, kulikuwa na ongezeko la mapato na faida kutokana na uwekezaji katika rasilimali na mtaji ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2019. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2020, faida ya benki itokanayo na mali (*Returns on Asset - ROA*) ilifikia wastani wa asilimia 2.18 na faida ya benki itokanayo na mtaji (*Returns on Equity - ROE*) ilifikia wastani wa asilimia 9.01 kutoka asilimia 1.80 na asilimia 7.66, mtawalia, Novemba 2019.

24. Thamani ya rasilimali za benki iliimarika kama inavyojidhihirisha katika mikopo chechefu ambayo ilipungua kufikia asilimia 10.16 Novemba 2020 kutoka asilimia 10.84 Novemba 2019. Mwenendo huu ulichochewa na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwa ni pamoja na: Kutoa maelekezo kwa benki kuendelea kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji (credit reference system) katika utoaji wa mikopo; kuimarisha mifumo ya udhibiti wa benki; benki kuendelea kuimarisha viwango vya uchambuzi wa maombi ya mikopo; kusimamia maadili ya wafanyakazi wa benki; kufanya ukaguzi maalum wa wafanyakazi (staff audit) wa benki mara kwa mara; na kuzielekeza benki na taasisi za fedha kutekeleza mikakati ya kupunguza mikopo

chechefu na kutoa taarifa kila robo mwaka.

### 1.4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

25. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Novemba 2020, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 818.6 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,661.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizouzwa nje pamoja na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

26. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Novemba 2020, mauzo ya bidhaa na huduma nje yalikuwa dola za Marekani milioni 8,839.9. Mauzo ya bidhaa asilia yalifikia dola za Marekani milioni 826.1 kutoka dola za Marekani milioni 745.1 Novemba 2019. Ongezeko hili lilitokana na mauzo ya korosho, pamba na karafuu lililochangiwa na ongezeko la uzalishaji wa mazao husika. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia (ambazo huchangia kwa asilimia 80 ya mauzo ya bidhaa nje) iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,160.7 kutoka dola za Marekani milioni 4,091.0 Novemba 2019, kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za mbogamboga, bidhaa za viwandani na madini. Mauzo ya dhahabu nje yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 2,855.6 kutokana na kuimarika kwa uzalishaji na bei katika soko la dunia.

27. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Novemba 2020, thamani ya bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ilipungua kufikia dola za Marekani milioni 8,966.4 kutoka dola za Marekani milioni 10,516.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kupungua kwa thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kulitokana na kushuka kwa uagizaji wa mitambo, na bidhaa za uzalishaji viwandani kutokana na kuathirika kwa usambazaji wa bidhaa hizo duniani kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

28. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma. Hadi Desemba 2020, kulikuwa na akiba ya fedha za kigeni ya dola za Marekani bilioni 4.8, ambayo inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 5.6. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 1.5 Deni la Serikali

29. Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 56,449.83 Juni 2020, ikilinganishwa na shilingi bilioni 53,240.95 Juni 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 15,515.74 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni

40,934.09. Mwenendo huo wa deni umetokana na kupokelewa kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayochochea uwezo wa kuzalisha mali, kukuza uchumi, kuongeza ajira na kulipa mikopo hiyo. Hadi Novemba 2020, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 58,407.06. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi bilioni 15,882.22 na la nje ni shilingi bilioni 42,524.84. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2020 imeonesha kuwa Deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo unaokubalika kimataifa kwa viashiria vyote muhimu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa thamani halisi ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70.

## 1.6 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Tanzania

### 1.6.1 Ukuaji wa Pato la Taifa

30. Uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.5 kwa mwaka 2020. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zinazotarajia kuwa na ukuaji chanya mwaka 2020 kutokana na hatua za Serikali za kutowafungia watu ndani na kuwaruhusu waendelee na shughuli za kiuchumi wakati wa mlipuko wa *COVID-19*. Aidha, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua na kufikia wastani wa asilimia 6.3 katika muda wa kati.

### 1.6.2 Mfumuko wa Bei

31. Mfumuko wa bei nchini Tanzania unatarajiwa kuwa na kiwango kisichozidi asilimia 5.0 katika muda wa kati. Aidha, Tanzania itaendelea kudhibiti mfumuko wa bei ili kuendana na vigezo (convergency criteria) vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Matarajio ya kasi ndogo ya mfumuko wa bei yanatokana na: kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya gesi na umeme; matarajio ya kuendelea kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia; sera madhubuti za fedha na bajeti; na matarajio ya upatikanaji wa chakula kwenye masoko ya ndani na nchi jirani kutokana na hali nzuri ya hewa nchini na ukanda wa Afrika Mashariki.

### 1.6.3 Malengo na Shabaha za Uchumi Jumla

32. Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2021 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 ifikapo mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika

muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 na asilimia 16.3 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/21;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0); na

(vii) Kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2019/20

## 2.1 Utangulizi

33. Sura hii inaelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2019/20 kwa kuzingatia mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi, mafanikio na changamoto ili kuboresha maandalizi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22. Aidha, mapitio ya utekelezaji yamefanyika katika baadhi ya miradi ya maendeleo ya kielelezo, kimkakati na maeneo mengine ya kipaumbele. Hivyo, mapitio haya yamefanyika kwa kulinganisha malengo na shabaha za kibajeti yaliyowekwa kwa kipindi husika.

## 2.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019/20

34. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20, ulizingatia vipaumbele vilivyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Agenda ya Afrika 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Katika kufikia malengo ya vipaumbele hivyo, Serikali ilitekeleza programu, miradi na sera mbalimbali zikiwemo kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati, kupanua wigo wa kodi na kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kuhimiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, Sera za matumizi zililenga kuelekeza fedha katika maeneo ya vipaumbele yenye kuchochea ukuaji wa uchumi, kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini katika matumizi, hususan katika miradi ya maendeleo.Vilevile, utekelezaji wa mpango na bajeti ulizingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

### 2.2.1 Mapato na Matumizi

#### 2.2.1.1 Mapato ya Ndani

35. Mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 20,290.2, sawa na asilimia 88.0 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 17,622.8 zilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania sawa na asilimia 92.3 ya lengo. Aidha, shilingi bilioni 1,950.2 ni mapato yasiyo ya kodi, sawa na asilimia 85.9 ya lengo na shilingi bilioni 717.2 ni mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, sawa na asilimia 93.7 ya lengo. Serikali itaendelea

kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa malengo ya mapato ya ndani yanafikiwa ikiwemo: Kuendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato, kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki za kutolea stakabadhi (EFD), kusimamia ukusanyaji kwa mfumo wa vitalu (Block management) na kutembelea walipa kodi mara kwa mara ili kuwapa elimu ya umuhimu wa kulipa kodi.

36. Katika mwaka 2020/21, Serikali imeanza kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kibajeti hususan katika kukokotoa, kuandaa maoteo ya mapato na matumizi ili kuiwezesha Serikali kuwa na bajeti endelevu ambapo pamoja na mambo mengine tathmini hii itaiwezesha Serikali kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, uchambuzi wa kina wa matumizi ya Serikali utafanyika ili kuongeza ufanisi endelevu katika utekelezaji wa bajeti.

**2.2.1.2 Misaada**

37. Katika mwaka 2019/20, Serikali ilipokea misaada ya shilingi bilioni 927.8 sawa na asilimia 76.8 ya lengo la shilingi bilioni 1,208.5. Kati ya kiasi hicho, Misaada ya Kibajeti ni shilingi bilioni 265.3 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 146.8, sawa na asilimia 180.7 ya lengo; Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 181.1 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 164.7, sawa na asilimia 109.9 ya lengo na misaada ya miradi ya maendeleo iliyopokelewa ni shilingi bilioni 481.4 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 896.9, sawa na asilimia 53.7 ya lengo. Kuvukwa kwa lengo kwa baadhi ya maeneo kulitokana na Washirika wa Maendeleo kuongeza viwango vya misaada waliyoahidi awali kutokana na mahusiano mazuri kati ya nchi yetu na Washirika hao wa Maendeleo.

**2.2.1.3 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti**

(a) **Mikopo Nafuu**

38. Kiasi cha shilingi bilioni 2,588.2 kilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 164.3 ya lengo la shilingi bilioni 1,575.2. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 126.1 sawa na asilimia 100.1 ya makadirio ya shilingi bilioni 125.9, Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 120.3 sawa na asilimia 346.1 ya makadirio ya shilingi bilioni 34.7, na mikopo ya miradi ni shilingi bilioni 2,341.9 sawa na asilimia 165.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,414.4.

(b) **Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara**

39. Katika mwaka 2019/20, Serikali ilikopa shilingi bilioni 1,822.1 kutoka vyanzo vya nje ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 2,316.4 sawa na asilimia 78.7 ya makisio. Kutofikiwa kwa lengo kumetokana na majadiliano ambayo yamechukua muda

mrefu pamoja na masharti magumu katika soko la mitaji la kimataifa. Aidha, Serikali ilikopa shilingi bilioni 4,960.0 kutoka masoko ya ndani sawa na asilimia 100.0 ya makadirio. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 3,976.8 zilikuwa ni kwa ajili ya kulipa mikopo iliyoiva na shilingi bilioni 983.2 zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo.

**2.2.1.4 Matumizi**

40. Katika mwaka 2019/20, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 33,105.4. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 20,810.3 fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 12,295.1 fedha za maendeleo. Hadi Juni 2020, jumla ya shilingi bilioni 28,573.1 zilitolewa sawa na asilimia 86.3 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, shilingi bilioni 1,462.6 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na shilingi bilioni 552.7 ni mapato yaliyopokelewa mwishoni mwa Juni 2020 na hivyo kupunguza nakisi ya Serikali (Government Position). Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 20,208.0 ni fedha za matumizi ya kawaida sawa na asilimia 96.9 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8,365.1 ni fedha za maendeleo kwa fedha zilizopitia Mfuko Mkuu wa Serikali, sawa na asilimia 68.3 ya bajeti ya maendeleo.

**(a) Matumizi ya Kawaida**

41. Matumizi ya kawaida yalijumuisha: Mishahara shilingi bilioni 7,297.2 sawa na asilimia 99.0 ya lengo la shilingi bilioni 7,373.3; deni la Serikali kwa fedha ambazo zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo shilingi bilioni 8,109.1, sawa na asilimia 100.0 ya lengo la shilingi bilioni 8,109.1; na matumizi mengineyo shilingi bilioni 4,801.7, sawa na asilimia 90.1 ya makadirio ya shilingi bilioni 5,328.0.

**(b) Matumizi ya Maendeleo**

42. Matumizi ya Maendeleo kwa fedha zilizopitia Mfuko Mkuu wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 8,365.1 sawa na asilimia 68.3 ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 6,678.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,686.4 ni fedha za nje. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 1,462.6 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na hivyo kufanya utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 80.2. Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa fedha zote za maendeleo kulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya upatikanaji wa mapato kama ilivyokadiriwa.

**2.2.2 Utekelezaji wa Bajeti Katika Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21**

43. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21, mapato yaliyokusanywa kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje ni shilingi bilioni 13,833.4 sawa na asilimia 87.3

ya lengo. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 10,449.0, sawa na asilimia 88.9 ya lengo. Kati ya mapato ya ndani: shilingi bilioni 9,045.5 zilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, sawa na asilimia 89.5 ya lengo; shilingi bilioni 1,027.0 ni mapato yasiyo ya kodi, sawa na asilimia 83.6 ya lengo; na shilingi bilioni 376.5 ni mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, sawa na asilimia 89.0 ya lengo. Aidha, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia kiwango cha juu ambacho hakijawahi kutokea cha shilingi bilioni 2,087.9 Desemba 2020. Misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 971.2, sawa na asilimia 63.1 ya lengo na mikopo kutoka masoko ya ndani shilingi bilioni 2,413.2, sawa na asilimia 94.6 ya lengo.

44. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 ilikuwa shilingi bilioni 13,120.9, sawa na asilimia 82.8 ya lengo. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 10,521.9 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 95.2 ya lengo na shilingi bilioni 2,599.0 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 54.2 ya lengo. Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 3,644.6 kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 97.7 ya lengo; shilingi bilioni 4,019.3 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali kwa fedha ambazo zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 92.9 ya lengo; na shilingi bilioni 2,858.0 kwa ajili matumizi mengineyo, sawa na asilimia 95.4 ya lengo. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 2,512.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 86.2 fedha za nje. Vile vile, kiasi cha shilingi bilioni 730.7 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na hivyo kufanya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 69.4.

### 2.2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti

45. Utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 umekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja na sekta mbalimbali. Mafanikio hayo ni pamoja na:

46. **Uchaguzi Mkuu:** Serikali kugharamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kutumia fedha za ndani ambapo jumla ya shilingi bilioni 268.5 zilitumika.

47. **Ukusanyaji wa Mapato:** Mapato ya kodi yaliongezeka hadi kufikia wastani wa shilingi bilioni 1,468.5 kwa mwezi, mwaka 2019/20 kutoka wastani wa shilingi bilioni 1,292.6 kwa mwezi, mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Aidha, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia kiwango cha juu ambacho hakijawahi kutokea cha shilingi bilioni 2,087.9 Desemba 2020. Ongezeko hili linatokana na juhudi zinazofanywa na Serikali ikiwemo kudhibiti upotevu wa mapato kwa

kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato.

48. **Ulipaji wa Mishahara:** Hadi Juni, 2020 jumla ya shilingi bilioni 7,297.2 sawa na asilimia 99.0 ya lengo la shilingi bilioni 7,373.3 zililipwa kwa wakati kwa kutumia mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi.

49. **Ulipaji wa Deni la Serikali:** katika mwaka 2019/20, Serikali ililipa shilingi bilioni 8,109.1 sawa na asilimia 100 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,777.8 zilitumika kulipa mitaji na shilingi bilioni 2,331.3 kulipa riba. Aidha, ulipaji wa deni kwa wakati kumewezesha Serikali kuendelea kuaminika katika Masoko na Taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi.

### 2.2.4 Mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati

50. **Ujenzi wa Reli ya Kati Kwa Kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge Railway*):** Serikali inaendelea na ujenzi wa reli ya kati ya kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway- SGR) ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 49.2, kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) wenye thamani ya shilingi trilioni 3.07; na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 901.8 zimetumika na shilingi bilioni 351.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

51. **Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere:** Katika mwaka 2019/20, Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa; kukamilika kwa handaki la kuchepushia maji; kuendelea na ujenzi wa mgodi wa kuzalisha umeme, ujenzi wa njia za kupeleka maji kwenye mitambo na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya mradi. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25.8. Utekelezaji wa mradi huu ulitumia shilingi bilioni 693.2 katika mwaka 2019/20 na shilingi bilioni 128.9 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

52. **Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania:** Serikali imekamilisha malipo ya mwisho ya ununuzi wa ndege aina ya Bombadier Dash 8-Q400 na Boeing 787-8 Dreamliner na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tatu (3), ambapo ndege mbili (2) ni aina ya Airbus A220-300 na moja (1) ni Dash 8-Q400 De-Havilland na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na ndege mpya 11 kutoka ndege moja (1) iliyokuwepo

mwaka 2015 na kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12 ambapo ndege tatu (3) zinatarajiwa kuwasili mwaka 2021/22. Aidha, Serikali imegharamia mafunzo kwa marubani 110, wahandisi 127 na wahudumu wa ndani ya ndege 131. Hatua hizi zimechangia kuimarika kwa huduma za usafiri wa anga kutoka vituo vinne (4) mwaka 2015 hadi vituo 13 vya ndani ya nchi na vituo saba (7) vya nje ya nchi mwaka 2020 na kuongezeka kwa idadi ya miruko ya ndege ndani na nje kutoka 225,103 mwaka 2015 hadi miruko 292,105 mwaka 2019. Katika mwaka 2019/20, shilingi bilioni 315.2 zimetumika na shilingi bilioni 2.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

53. **Viwanja vya Ndege na Rada:** Kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere – JNIA chenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita (6) kwa mwaka; kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Geita (asilimia 86), Songea (asilimia 91) na Mtwara (asilimia 49); kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambao utagharimu dola za Marekani milioni 330, sawa na shilingi bilioni 759; uzinduzi wa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85; kuanza kwa ujenzi na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Musoma; kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege na kununuliwa kwa magari mapya matatu (3) ya zimamoto yenye uwezo wa kubeba lita za maji 10,000 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA); kuendelea kukamilisha upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kufungwa kwa mifumo ya kuongoza ndege (AGL) katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza; na kupanuliwa na kukarabatiwa kwa viwanja vya ndege vya Bukoba, Mwanza, Arusha, Nachingwea na Iringa. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 56.1 zimetumika na shilingi bilioni 4.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha shilingi bilioni 404.0 kimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya viwanja vya ndege.

54. **Usambazaji wa Umeme Vijijini:** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini kwa lengo la kuhakikisha vijiji vyote Tanzania Bara vinafikiwa na huduma ya umeme. Hadi Desemba 2020, jumla ya vijiji 10,018 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 81.3 vilikuwa vimeunganishiwa umeme. Katika mwaka 2019/20, shilingi bilioni 323.7 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/21 shilingi bilioni 171.9 zimetolewa.

55. **Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – (LNG):** Serikali iliendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kusindika Gesi Asilia nchini. Katika mwaka 2019/20, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi ambapo jumla ya shilingi bilioni 5.2 zimetumika; na kuanza majadiliano ya Mikataba Hodhi baina ya Serikali na Kampuni za uendelezaji mradi.

56. **Usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza; kupatikana kwa makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti na kukamilika kwa maandalizi ya mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli hizo; na kukamilika kwa ukarabati wa meli za MV Clarias na ML Wimbi. **Ziwa Tanganyika:** kukamilika kwa mikataba kwa ajili ya Ujenzi wa Meli Mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba; na ukarabati wa meli ya MT Sangara ambapo katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 53.5 zimetumika na shilingi bilioni 12.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

57. Shughuli nyingine zilizokamilika ni: Ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na Gati la majahazi Mwigobero; ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli; ukarabati wa majengo na Ofisi za Bandari za Ziwa Victoria; kuboresha eneo la kushukia abiria Mwanza North; na ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 2.7 zimetumika.

58. **Ziwa Nyasa:** Kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja; na ujenzi wa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 umekamilika na kuanza kufanya kazi. Katika mwaka 2019/20, shilingi milioni 233.9 zimetumika na shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

59. **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** Kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 3,537 (barabara kuu na za mikoa kilomita 2,209 na barabara za Halmashauri kilomita 1,328) na hivyo kufanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/20 kufikia kilomita 13,044 ambapo kilomita 10,939 ni barabara kuu na kilomita 2,105 ni barabara za mikoa. Ujenzi huu umeongeza uwiano wa mtandao wa barabara za lami nchini kutoka asilimia 6.8 mwaka 2015/16 hadi asilimia 8.9 mwaka 2019/20.

60. Miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85), Manyoni - Itigi – Chaya (km 89.35), Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52) na Kaliua – Kazilambwa (km 56); kukamilika kwa barabara ya Mpanda - Ifukutwa - Vikonge (km 30); kukamilika kwa barabara ya Kidahwe - Kasulu (km 63); kukamilika kwa ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110); kuzinduliwa na kuanza kutumika kwa barabaya ya juu (Interchange) ya Ubungo; kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Mfugale (Dar es Salaam); ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kakonko (km 50) umefikia asilimia 90.8; ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta umekamilika kwa asilimia 86.0; ujenzi kwa sehemu ya Mbinga - Mbamba Bay (km 66) utekelezaji umefikia asilimia 85.5 na sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) asilimia 90; na kukamilika kwa asilimia 92.9 ya upanuzi wa barabara sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2); kuendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) lenye urefu wa kilomita 3.2 na upana wa mita 28.45 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5.8.

61. Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa 12 ambayo ni Magufuli (Morogoro), Nyerere (Dar es Salaam), Magara (Manyara), Kavuu (Katavi), Ruvu Chini (Pwani), Mlalakuwa (Dar es Salaam), Momba (Rukwa), Lukuledi (Lindi), Lukuledi II (Lindi), Mara (Mara), Sibiti (Singida) na Mtibwa (Morogoro); kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Ruhuhu (Ruvuma) asilimia 95, Mitomoni (Ruvuma) asilimia 75; Daraja jipya la Tanzanite (Dar es Salaam) asilimia 55.2; Kitengule (Kagera) asilimia 50; na New Wami (Pwani) asilimia 41.4.

62. Ongezeko la mtandao wa barabara na ujenzi wa madaraja umerahisisha usafirishaji wa bidhaa na mazao ya kilimo, malighafi na bidhaa za viwandani pamoja na huduma ya usafiri kwa wananchi katika maeneo yaliyokuwa hayafikiki. Katika mwaka 2019/20, shilingi trilioni 1.93 zilitumika na shilingi bilioni 398.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

63. **Uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma**: Serikali imeanza maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba yatakayotosheleza watumishi wote. Katika mwaka 2019/20, Serikali imekamilisha usanifu wa majengo husika. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (km 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 89.13 unaendelea, ambapo malipo ya awali ya shilingi bilioni 13.21 yamefanyika.

64. **Miradi ya Vivuko:** Hadi Desemba 2020 serikali ilitoa shilingi bilioni 14.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya vivuko. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kukamilisha

ujenzi wa vivuko vipya vya Kigongo - Busisi (Mwanza), Bugolora – Ukara (Mwanza) na Kayenze – Bezi (Mwanza). Aidha, ujenzi wa kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 100 na Chato – Nkome (Geita) asilimia 100. Vilevile, ujenzi wa boti mpya tano (5) za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), kivuko cha Magogoni – Kigamboni na Lindi – Kitunda unaendelea. Pia ukarabati mkubwa wa MV Kigamboni na kivuko cha MV Sengerema umekamilika.

65. **Kilimo:** Kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Kigugu – Mvomero yenye hekta 200 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, Mvumi – Kilosa yenye hekta 249 (asilimia 100), Msolwa Ujamaa – Morogoro yenye hekta 675 (asilimia 98), Njage – Kilombero yenye hekta 325 (asilimia 100), Shamba la Mbegu Kilangali – Kilosa yenye hekta 400 (asilimia 80); kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 71,000 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – Morogoro; kuzalishwa kwa kilo 14,700 za mbegu za mpunga za daraja la awali (*pre-basic*) aina ya TXD 306, TXD 88, Komboka, Tai, Supa na NERICA 1; kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,450 mwaka 2015 hadi tani 727,719 mwaka 2020; kukamilisha ujenzi wa maghala matano (5) ya kuhifadhi mpunga kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga – *Expanded Rice Production Project*; kusambazwa kwa tani 40,592.6 za salfa na lita 1,314,465 za viuatilifu maji kwa wakulima wa korosho; kuendeshwa kwa minada nane (8) ya kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro (2), Songwe (4) na Ruvuma (2); na kukaguliwa kwa viwanda 24 na maghala 30 na kutolewa leseni za kuendesha biashara ya kahawa. Hatua hizi zimechangia kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 118 mwaka 2019/20; kupungua kwa mfumuko wa bei za chakula kufikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2020; na kupungua kwa Umaskini wa Chakula kufikia asilimia asilimia 8.0 mwaka 2018. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 45.9 zimetumika na shilingi bilioni 57.1 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

66. **Mifugo:** Kujengwa kwa kiwanda kipya cha *Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd* chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka na kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka; kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha *National Artificial Insemination Center* - NAIC kilichopo USA River Arusha kwa kununua kifaa (Chiller) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha

naitrojeni; kujengwa kwa viwanda vipya vya kimkakati vya nyama vya *Tanchoice* (Pwani), *Elia Food Oversees Limited* (Arusha) na *Binjiang Company Limited* (Shinyanga); kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverage Company Limited* (Arusha); kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha *Hester Bioscience Africa Limited* (Pwani) chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37; na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho.

67. Utekelezaji huu umewezesha mafanikio yafuatayo: kuongezeka kwa viwanda vya kusindika nyama nchini kutoka 25 mwaka 2015/16 hadi viwanda 32 mwaka 2019/20 na viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 mwaka 2015/16 hadi 99 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa usambazaji wa mitamba katika mashamba ya Serikali kutoka mitamba 11,449 mwaka 2015/16 hadi mitamba 18,255 mwaka 2019/20; kuongeza idadi ya majosho ya kuogeshea mifugo kutoka majosho 2,428 mwaka 2015/16 hadi majosho 2,513 mwaka 2019/20; kuongezeka maeneo ya malisho ya mifugo kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015/16 hadi hekta milioni 2.85 mwaka 2019/20; kuendelea kukamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa Vingunguti; na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na zao la ngozi kutoka shilingi bilioni 1.73 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 9.1 mwaka 2019/20. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 2.76 zimetumika na shilingi bilioni 1.77 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/21.

68. **Uvuvi:** Kuongezeka kwa uzalishaji/uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2015/16 hadi tani 497,567 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya Sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/16 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/20, jumla ya kilo 777,750.0 za mabondo zilisafirishwa; kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.25 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 506.24 mwaka 2019/20; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi (Mbegani). Katika mwaka 2019/20 shilingi milioni 426.3 zimetumika na shilingi milioni 606.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/21.

69. **Uchumi wa Bahari:** Katika mwaka 2019/20, Serikali ilitoa shilingi milioni 149.7 kwa ajili ya kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania. Aidha, Serikali iliingia mkataba wa msaada wa vifaa vya uvuvi vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.2. Vifaa hivyo ni pamoja na: meli ya uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu; mtambo wa kuzalisha barafu; gari maalum la kubeba samaki; na kukarabati ghala la kuhifadhia samaki.

70. **Madini:** Kupitia na kutunga Sheria, Sera na mikataba ya madini; kuanzishwa kwa Kampuni mpya ya Twiga Minerals Corporation inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (hisa asilimia 16) na Kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84) ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kusainiwa kwa mkataba wa ubia wa kampuni ya LZ NICKEL na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza na kuchimba madini ya Nickel ambapo chini ya mkataba huo imeundwa kampuni ya ubia inayoitwa Tembo Nickel Corporation Limited (kwa umuliki wa hisa 84% kwa Kampuni ya LZ Nickel na Serikali ya Tanzania Hisa 16%); kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali za madini kwa kujenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24 wa Mirerani Manyara pamoja na kujenga *one stop centre*, kufunga vifaa vya ulinzi ikiwa ni pamoja na taa na *CCTV Camera* kuzunguka ukuta na barabara ya kuzunguka ukuta wa ndani; kuimarisha taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuzipatia vitendea kazi; na kukamilisha ujenzi wa Vituo Vitatu (3) vya Mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya). Jitihada hizi zimechangia Sekta ya Madini kukua kwa wastani wa asilimia 8.0 kati ya mwaka 2016 na 2019; mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 4.6 mwaka 2015/16 na kuimarika kwa huduma kwa jamii zinazozunguka migodi. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,912 (sawa na shilingi bilioni 4,464.71) mwaka 2015/16 hadi dola za Marekani milioni 2,898.8 (sawa na shilingi bilioni 6,769.0) mwaka 2019/20; na maduhuli kutoka shilingi bilioni 196 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 528.3 mwaka 2019/20. Kadhalika, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 jumla ya shilingi bilioni 317.5 zimekusanywa, sawa na asilimia 120.6 ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 263.4. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 3.08 zimetumika, na shilingi bilioni 3.3 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/21 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

71. **Miradi ya Maji:** Kukamilika kwa miradi 1,423 ya maji iliyotekelezwa mijini na vijijini. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua zilizofikiwa ni: kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma (asilimia 90); utekelezaji wa Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega umefikia asilimia 98; kukamilika kwa asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza; kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji

katika Jiji la Arusha; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 65. Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na umehusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe-Pugu-Ukonga, Mbezi Luis, Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo (maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga na Kerege).

72. Kwa ujumla miradi yote iliyotekelezwa imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma ya maji ambapo wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020 kwa mijini na kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020 kwa vijijini. Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam, upatikanaji wa maji safi umeongezeka kutoka asilimia 72 mwaka 2015 hadi asilimia 90 Desemba, 2020. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 511.5 zimetumika na shilingi bilioni 226.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/21.

73. **Elimu**: Kujengwa kwa miundombinu muhimu katika shule 3,904 (Msingi 3,021 na Sekondari 883), mabweni 547, nyumba za walimu 101, majengo ya utawala 25 na maktaba 43; kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133; kuendelea kugharamia posho ya madaraka kwa walimu wakuu, fidia ya ada kwa wanafunzi na ruzuku ya uendeshaji wa shule; kukarabatiwa shule kongwe 84 kati ya 89; kuboreshwa kwa miundombinu ya vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (*Folk Development Colleges - FDC*); kuanzishwa kwa vituo vya umahiri vya mafunzo katika taasisi za elimu ya ufundi; na kuimarishwa kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika taaluma za Anga na Chuo cha Ufundi Arusha katika taaluma ya Nishati; na kukamilika na kuzinduliwa kwa Maktaba ya Kimataifa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,600 kwa wakati mmoja pamoja na hosteli za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

74. Hatua hizi zimechangia: kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimumsingi kutoka asilimia 91.9 mwaka 2015 hadi asilimia 110.3 ya lengo mwaka 2019; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 196,091 mwaka 2015/16 hadi 320,143 mwaka 2019/20 na elimu ya ufundi kutoka 117,067 mwaka 2015/16 hadi 151,379 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015 hadi kufikia 87,813 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya

juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015 hadi kufikia 132,392 mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ufaulu mitihani ya Darasa la Saba kimeongezeka kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 mwaka 2019 na Sekondari (Kidato cha nne) kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 80.7 mwaka 2019. Vilevile, wanafunzi waliohitimu elimu ya juu walifikia 60,940 mwaka 2019/20, elimu ya mafunzo stadi 90,849 mwaka 2018/19 na elimu ya ufundi 86,547 mwaka 2019/20. Katika mwaka 2019/20, shilingi bilioni 734.9 zimetumika na shilingi bilioni 159.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

75. **Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu:** Hadi Juni 2020, Serikali imetekeleza yafuatayo: kutambua na kuhakiki teknolojia 231 zilizoanzishwa na wabunifu wa ndani kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa kuhusu teknolojia; kuwaendeleza wabunifu 60 waliopatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo bunifu 12 zipo katika hatua ya kutengeneza bidhaa za mfano; kukamilisha hatua ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya yenye uwezo wa kuwahudumia wanafunzi 2,500; na kutekeleza miradi 332 ya utafiti katika Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti. Aidha, kuwaendeleza wabunifu 131 ili ubunifu wao uweze kuingia sokoni, kutambua wabunifu wapya wachanga 1,066 na kutoa vibali vya utafiti 449.

76. **Afya**: kuendelea kutoa huduma za kupandikiza uloto (*bone marrow transplant*) na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wodi namba 18 ya Sewa Haji pamoja na ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa binafsi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la *X-ray* katika Hospitali ya Rufaa Dodoma; kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru – Dodoma na kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje; kununuliwa kwa mashine za *digital X-ray* na *ultrasound*, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea BACTEC 960 (*Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT*) na *Blood culture machine* katika Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto; ununuzi wa mashine ya *Positron Emmission Tomography* (PET Scan) kwa ajili ya Hospitali ya Ocean Road; kujenga na kuboresha miundombinu ya hospitali za rufaa za Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekou Toure (Mwanza), hospitali za rufaa za kanda ya kusini Mtwara, kanda ya nyanda za juu kusini Mbeya, Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) na Hospitali ya Kanda ya Ziwa ya Burigi (Geita).

77. Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya ambayo imefikia hatua mbalimbali ikiwemo: kufikia asilimia 98 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto

katika Hospitali ya Rufaa Mwananyamala; kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la wagonjwa wa nje na kufikia asilimia 73 ya ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa Njombe; na ujenzi wa jengo la huduma za upasuaji, radiolojia na maabara na kufikia asilimia 50 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Simiyu. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na: ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; na kuongezeka kwa idadi ya zahanati kutoka 4,922 mwaka 2015 hadi 6,120 mwaka 2020, vituo vya afya kutoka 535 mwaka 2015 hadi vituo 710 mwaka 2020 na Hospitali za Halmashauri za Wilaya kutoka 77 mwaka 2015 hadi 179 mwaka 2020.

78. Hatua hizi zimechangia: Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 62 mwaka 2015/16 hadi miaka 66 mwaka 2019/20; kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2015/16 hadi vifo 50 mwaka 2019/20; kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 mwaka 2015/16 hadi asilimia 80 mwaka 2019/20. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 321.24 zimetumika na shilingi bilioni 64.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

79. **Viwanda:** Kujengwa kwa jumla ya viwanda vipya 8,477 kati ya mwaka 2015 – 2019 ambapo viwanda vikubwa ni 201, vya kati 460, vidogo 3,406 na vidogo sana 4,410. Ujenzi wa viwanda hivyo, umeongeza idadi ya viwanda nchini kutoka 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2019. Viwanda hivyo vimechangia ongezeko la uzalishaji wa bidhaa kwa soko la ndani na la nje ikijumuisha bidhaa mbalimbali zikiwemo za ngozi, bidhaa za ujenzi (nondo, mabati, saruji, misumari na rangi), plastiki, zana za kilimo, vinywaji na marumaru. Baadhi ya viwanda vilivyojengwa ni: *Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd* (awamu ya kwanza ya kiwanda kipya cha bidhaa za ngozi) katika mkoa wa Kilimanjaro; kiwanda cha *Pipe Industries Co. Limited* kinachozalisha mabomba kilichopo Vingunguti, Dar es Salaam; majengo ya viwanda (Industrial Sheds) kwa ajili ya wajasiriamali katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Geita, Mtwara na Ruvuma; kiwanda cha chai cha Kabambe (Njombe); kiwanda cha *Yalin Cashewnut Company Ltd* kinachobangua korosho (Mikindani – Mtwara); viwanda vya *Goodwill Tanzania Ceramic Co. Ltd* na Keda (T) *Ceramics Company Ltd* vilivyopo mkoa wa Pwani vinavyozalisha marumaru; kiwanda cha *Plasco Pipelines Co. Ltd (Dar es Salaam)* kinachozalisha bidhaa za plastiki; kiwanda cha *Africa Dragon Enterprises Limited* (Pwani) kinachozalisha mabati; na jengo la kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta

TAMCO – Kibaha.

80. Uwekezaji huo umeleta mafanikio yafuatayo: Kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015 hadi asilimia 8.5 mwaka 2019**;** kukua kwa sekta ya uzalishaji viwandani kwa wastani wa asilimia 8.3 kwa mwaka; kuzalishwa kwa fursa za ajira kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi ajira 482,601 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 47.2; na kuchangia katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 13.8 mwaka 2016/17 hadi asilimia 14.2 mwaka 2019/20. Katika mwaka 2019/20 na nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 shilingi bilioni 5.5 zimetumika .

81. **Maliasili na Utalii:** Kujengwa na kukarabatiwa viwanja vya ndege; kununuliwa kwa ndege; kuongezwa kwa safari za ndege ndani na nje ya nchi; kudhibiti ujangili, kuongeza idadi ya watalii na mapato kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo katika Hifadhi za Taifa, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili na Mradi wa Kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW); na kutangazwa kwa vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali duniani. Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,527,230 mwaka 2019. Aidha, wastani wa idadi ya siku zinazotumiwa na watalii nchini zimeongezeka kufikia siku 13 mwaka 2019 ikilinganishwa na siku 10 mwaka 2015. Mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.9 (sawa na shilingi bilioni 4,436.7) mwaka 2015 hadi dola za Marekani bilioni 2.6 (sawa na shilingi bilioni 6,071.3) mwaka 2019. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 14.5 zimetumika, na shilingi bilioni 5.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya 2020/21.

82. **Katiba na Sheria:** Katika kuimarisha utawala bora, Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuboresha utoaji haki na upatikanaji wa huduma za kisheria kwenye maeneo yafuatayo:

(i) **Mahakama:** Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 10.2 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama na nyumba za majaji. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa: majengo mawili (2) ya mahakama kuu ya Kigoma na Mara; majengo manne (4) ya mahakama ya Hakimu Mkazi Geita, Simiyu, Njombe na Manyara; majengo saba (7) ya mahakama za wilaya za Chato, Bukombe, Kilwa, Ruangwa, Kondoa, Chunya na Longido; majengo matano (5) ya mahakama za mwanzo zilizopo Mkunya – (Newala); Ngerengere (Morogoro), Msanzi na Mtowisa (Sumbawanga) na Uyole – (Mbeya); na nyumba nne (4) za makazi kwa ajili ya majaji (mbili (2) Kigoma na mbili (2) Musoma). Aidha, miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na: ukarabati wa

jengo la mahakama kuu Sumbawanga; Ujenzi wa majengo sita (6) ya vituo vya kutoa ushauri wa kisheria Arusha, Dodoma, Dar es Salaam (Temeke na Kinondoni), Mwanza na Morogoro; ujenzi wa mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi na Lindi; mahakama za wilaya ya Sikonge, Kilindi, Rungwe, Bunda, Makete, Wanging'ombe, Ludewa, Chemba, Bahi na Mji Mdogo Kibaigwa; Mahakama za mwanzo Mlimba na Mang'ula (Morogoro); na Mtae (Lushoto).

(ii) **Marekebisho ya Sheria**: Kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi na kuanzisha Kituo cha Usuluhishi cha Tanzania; marekebisho ya sheria mbalimbali yaliyolenga kuweka mifumo bora ya upatikanaji na ufikiwaji wa haki; kukamilika kwa Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Uangalizi wa Utajiri wa Asili na Maliasilia za Nchi (2019/20 - 2021/22); kutungwa kwa Kanuni za Sheria za Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Utajiri na Maliasilia za Nchi (GN. 58) na Kanuni za Maadili ya Wawekezaji (GN 59); na kufanyika kwa mapitio na utafiti katika mifumo minne (4) ya kutoa haki ya sheria.

(iii) **Usajili wa Mashauri**: Katika mwaka 2019/20, Serikali imesajili mashauri 3,111, ambapo mashauri 3,025 ni ya madai ndani na nje ya nchi na mashauri 86 ni ya usuluhishi. Kati ya mashauri yaliyosajiliwa, mashauri 427 yamemalizika na mengine yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Katika mashauri yaliyomalizika, Serikali imeshinda kesi za madai zenye thamani ya shilingi bilioni 249.24 na kesi za usuluhishi zenye thamani ya shilingi trilioni 11.13.

83. **Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato Katika Halmashauri:** Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao, Serikali ilitoa shilingi bilioni 91.4 kwa ajili ya kugharamia miradi 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50.6 zilitolewa mwaka 2019/20. Miradi ya ujenzi iliyotekelezwa ni pamoja na; stendi za mabasi (9), machinjio (2), viwanda vidogo (3), maegesho ya malori (2), masoko (9) na ghala la mazao (1). Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2020/21, Serikali imetoa shilingi bilioni 19.9 kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati.

### 2.2.4 Mafanikio Mengine Yaliyopatikana

84. **Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji pamoja na Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint*):** Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango huu ni pamoja na: Kufutwa kwa tozo, faini na ada mbalimbali 232; kuondoa muingiliano kwenye Mamlaka za Uthibiti za Mamlaka ya Maabara na Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Mamlaka ya Chakula

na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika utoaji wa vibali vya chakula, vipodozi na kusafirisha kemikali; na kuunganisha mifumo ya kielektroniki katika Taasisi ambapo Mfumo wa Malipo ya Serikali (Government Electronic Payment Gateway - GePG) umeunganishwa na mifumo mingine.

85. Utekelezajii wa Blueprint ulikuwa na mafanikio mengine yakijumuisha: Kuweka Miongozo na Taratibu za Utoaji Huduma (*Standard Operating Procedures- SOPS):* kuanzisha na kuimarisha vituo vya pamoja vya kutoa huduma kupitia TIC: kusogeza huduma karibu na watumiaji kwa taasisi nyingi kufungua na kuimarisha Ofisi za Kanda; kuboresha mifumo ya ukaguzi wa pamoja kwa kushirikisha Taasisi mbalimbali; na kutungwa Kwa Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020. Hatua hizi zimeimarisha utoaji wa huduma hususan za vibali na leseni; kupunguza urasimu na gharama za ufanyaji biashara; kupunguza mianya ya rushwa; na kuongeza dhana ya uwajibikaji kwenye Mamlaka za Udhibiti pamoja na kuongeza mapato kwa Serikali.

86. **Programu ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi:** Katika mwaka 2019/20, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Ubia kwa kutekeleza yafuatayo: kukamilisha Kanuni na Miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa Sheria ya PPP; kukamilisha muundo wa Kituo cha Ubia (*PPP Centre);* jumla ya miradi 12 inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ilipokelewa na kuchambuliwa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Hosteli, miradi ya Maji kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Moshi, Mwanza, Tanga na Mbozi – Songwe; miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano na Jengo la Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro; na mradi wa kujenga na kuendesha kiwanda cha kutengeneza simu za kiganjani. Aidha, miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi zikiwemo za kukamilisha taratibu za ununuzi na hatimaye kutangazwa ili kupata wabia. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa viwanda vitatu vya dawa na vifaa tiba; Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza (DART); na mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

87. **Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo:** Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na; kuchangia ukamilishaji wa miradi ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali zikiwemo elimu, afya, maji na ustawi wa jamii. Baadhi ya miradi iliyochangiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu na vituo vya afya ili kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2019/20, jumla ya shilingi bilioni 11.0 zilitolewa kwa ajili ya Mfuko huo.

88. **Uendelezaji wa Bandari:** Katika **Bandari ya Dar es Salaam** shughuli zilizofanyika ni: Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 4 (gati namba 1-3 kwa ajili ya mizigo mchanganyiko na gati namba 4 kwa ajili ya mizigo ya kichele mfano ngano na mbolea); kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari (RoRo); na kuendelea na uboreshaji wa gati na 5 hadi 7 (gati namba 5 kwa ajili ya mizigo ya kichele na gati namba 6-7 ni kwa ajili ya makontena). Hatua hizi zimechangia kupungua kwa idadi ya siku za meli kukaa bandarini kutoka siku saba (7) hadi siku tano (5) na kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 15.4 hadi tani milioni 19.52. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 207.6 zimetumika na shilingi bilioni 42.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

89. Katika **Bandari ya Mtwara** ujenzi wa gati jipya lenye urefu wa mita 300 na yadi ya kuhudumia makasha umekamilika ambapo katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 43.6 zimetumika na shilingi bilioni 44.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21. Aidha, katika **Bandari ya Tanga** ujenzi wa kina cha lango la bandari kutoka mita nne (4) hadi mita 13 na ujenzi wa gati mbili (2) kwenye kina kirefu umekamilika. Katika mwaka 2019/20 shilingi bilioni 66.5 zimetumika na shilingi bilioni 20.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21.

90. **Uendelezaji wa Sekta ya Fedha:** Serikali iliendelea kutekeleza Sera na Mikakati ya Kitaifa ya kuwezesha Maendeleo ya Sekta ya Fedha nchini na kuimarisha huduma za fedha zikiwemo huduma za Benki, Bima, Masoko ya Mitaji na Dhamana, Mifuko ya Hifadhi za Jamii pamoja na huduma ndogo za fedha hususani kwa wananchi wa kipato cha chini. Hadi Desemba, 2019 mitaji katika maeneo haya ulikuwa kama ifuatavyo: Benki (shilingi bilioni 33,083.5); Bima (shilingi bilioni 936.0); Masoko ya Mitaji na Dhamana (shilingi bilioni 19,676.92); Mifuko ya Hifadhi za Jamii (shilingi bilioni 12,000.8). Aidha, katika kipindi hicho kulikuwa na Taasisi za Watoa huduma ndogo za fedha 35,285 na Vikundi vidogo vya Kijamii 30,240 vyenye mtaji wa shilingi bilioni 58.9.

91. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa Mpango Mkuu wa Miaka Kumi wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha 2020/21-2020/30, kuunganishwa kwa Benki za Biashara ya TIB na Benki ya TPB; kuandaa mapendekezo ya kutunga Sera ya Taifa ya Benki, kuandaa mapendekezo ya kutunga Sera ya Taifa ya Bima, kuandaa mapendekezo ya kuanzisha utoaji wa hatifungani kwa kutumia simu za viganjani (M-Akiba); kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mikopo Salama; kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Huduma ndogo za Fedha na kukamilika kwa Kanuni za jumla za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2019.

92. **Usambazaji wa Gesi Asilia:** Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia nchini kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa: ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia yenye urefu wa km 18 na uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi Juni, 2020, wateja wapatao 500 wa majumbani na viwanda 48 vimeunganishwa kwenye miundombinu ya gesi na magari zaidi ya 400 yanatumia gesi asilia; ujenzi wa miundombinu ya gesi yenye urefu wa km 6 na uwezo wa kuunganisha viwanda zaidi ya 20 katika eneo la Mkuranga mkoani Pwani; ujenzi wa *trunk-lines* zenye urefu wa km 17 na uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 3,000 kwa Mkoa wa Mtwara.

93. **Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania):** Hadi Desemba 2020, hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa Tathmini ya Athari za Mazingira; kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi huo; na kukamilisha majadiliano ya mikataba ikiwemo ya nchi Hodhi na Wawekezaji.

### 2.2.5 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti

94. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/20**,** changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

(i) Uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mafuriko;
(ii) Kupungua kwa shughuli za kibiashara duniani kutokana na athari za *COVID-19*;
(iii) Ukwepaji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida (transfer pricing) kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika;
(iv) Kutosimamia kikamilifu mapato yanayokusanywa kwa baadhi ya Halmashauri; na
(v) Baadhi ya wazabuni kushindwa kutumia Mfumo wa TANePS kutokana na Mfumo huo kutoruhusu baadhi ya taarifa kuingizwa wakati wa maombi ya zabuni.

### 2.2.6 Hatua Zinazochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti

95. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza mapato na kuendelea kutatua changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa hatua hizo ni:

(i) Kuendelea kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga na kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko pamoja na kuimarisha ukaguzi

wake;

(ii) Kuendelea kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa biashara duniani ili kutumia fursa zilizotokana na athari za *COVID-19* kwa manufaa mapana ya nchi pamoja na kuchukua hatua za kisera na kiutawala kurejesha biashara zilizoathirika;

(iii) Kuendelea na hatua za kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara stahimilivu ili kuimarisha ushindani katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo utalii na kuongeza matumizi ya TEHAMA;

(iv) Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato vya ndani, masoko ya bidhaa nje na kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia bajeti yake;

(v) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato katika halmashauri kwa njia ya kielektroniki kwa kuongeza matumizi ya POS ambazo sio rahisi kufanyiwa udukuzi;

(vi) Mamlaka zinazokusanya mapato ya Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama katika kufanya doria maeneo ya mipaka ya nchi kavu, baharini na kwenye maziwa ili kudhibiti biashara za magendo;

(vii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya matumizi ya stakabadhi za kielektroniki (*Electronic Fiscal Devices – EFD*); na

(viii) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa Ununuzi Serikalini (TANePS) kwa kutoa mafunzo kwa wazabuni na maboresho ya kimfumo.

## SURA YA TATU

## MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

### 3.1 Utangulizi

96. Sura hii inaainisha sera za kibajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2021/22 na katika muda wa kati. Kwa mujibu wa Kifungu 21(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, Serikali ina wajibu wa kuandaa na kutekeleza sera wezeshi za kibajeti ili kuchochea uwekezaji, ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Aidha, sera hizo zinalenga kutekeleza dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu* ".

### 3.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla

97. Malengo na Shabaha ya uchumi jumla yanatarajiwa kuwa kama ifuatavyo: ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2021; mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5.0 kwa mwaka 2021/22; Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/22; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 3.3 Misingi ya Uchumi Jumla (Assumptions)

98. Misingi itakayozingatiwa kufikia shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani; kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko na magonjwa ya mlipuko; ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi; hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada; na kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa.

### 3.4 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati

#### 3.4.1 Sera za Mapato ya Ndani

99. Sera za mapato ya ndani katika muda wa kati zinalenga kuongeza makusanyo kwa kuendelea :

(i) Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwianisha na kufuta au kupunguza viwango vya kodi,

tozo na ada zinazoonekana kuwa kero ;

(ii) Kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa mikakati na miradi ya kuongeza mapato;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na

(v) Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na upanuzi wa wigo wa kodi.

### 3.4.2 Makadirio ya Mapato ya Ndani

100. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 26,032.6 mwaka 2021/22 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 24,065.5 mwaka 2020/21. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 8.6 hadi shilingi bilioni 30,852.1 mwaka 2023/24. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 69.0 mwaka 2020/21 hadi asilimia 71.8 mwaka 2021/22 na kuongezeka hadi asilimia 76.7 mwaka 2023/24. Mchanganuo wa mapato ya ndani ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.1.**

**Kielelezo Na. 3.1: Makadirio ya Mapato ya Ndani katika Muda wa Kati**

Shilingi bilioni




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

101. Katika mwaka 2021/22, mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 6.6 hadi shilingi bilioni 21,468.2 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 20,136.0 mwaka 2020/21. Katika muda wa kati, mapato ya kodi yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.8 hadi shilingi bilioni 25,256.1 mwaka 2023/24. Mapato ya kodi kwa Pato la Taifa yanakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 13.3 katika muda wa kati.

102. Katika muda wa kati, mapato yasiyo ya kodi yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 3,929.6 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 4,564.3 mwaka 2021/22 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 5,596.0 mwaka 2023/24. Mapato hayo yanakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 2.9 ya Pato la Taifa katika muda wa kati. Mchanganuo wa mapato yasiyo ya kodi ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.2.**

**Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi katika Muda wa Kati**

Shilingi bilioni




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

103. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mahsusi ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani. Mikakati hiyo ni pamoja na:

(i) Kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipakodi wapya kwa kutumia TEHAMA na kanzidata za taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Ofisi ya Taifa

ya Takwimu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA);

(ii) Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia kwa kuimarisha na kujenga mifumo wezeshi ya TEHAMA ili kurahisisha ulipaji wa kodi na uwasilishaji wa ritani za kodi;

(iii) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashine za kutolea stakabadhi za kielektorniki (EFD) kwa lengo la kupata taarifa na takwimu halisi za mienendo ya biashara ikiwa ni pamoja na kuweza kuhakiki madai ya marejesho ya VAT;

(iv) Kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Compliance Risk Management Plan) ili kuongeza uhiari wa ulipaji kodi;

(v) Kuanza kutumia Mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Tanzania (Tanzania Electronic Single Window System - TeSWs) ili kurahisisha upitishaji wa mizigo inayoingia na kutoka kupitia vituo vya forodha mipakani na hivyo kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;

(vi) Kuboresha Mfumo wa Serikali wa Kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG), kuhimiza matumizi ya Control Number na kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinatumia mfumo huo katika kukusanya mapato;

(vii) Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa mipaka yote na kuongeza ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na vyombo vya ulinzi na usalama nchini ili kupunguza tatizo la ukwepaji kodi;

(viii) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya Mashirika kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali inawasilishwa kwa wakati; na

(ix) Kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS) na kuunganisha Mfumo huu na mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kudhibiti upotevu wa mapato.

### 3.5 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati

#### 3.5.1 Sera za Matumizi

104. Sera za Matumizi katika muda wa kati zitajumuisha yafuatayo: -

(i) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;

(ii) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kuendana na vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iii) Kudhibiti ulimbikizaji wa madeni;

(iv) Kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; na

(v) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalam wa ndani kwenye eneo la usalama wa mifumo (systems security).

**3.5.2 Makadirio ya Matumizi**

105. Katika mwaka 2021/22 matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.0 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 34,879.8 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 36,258.8, sawa na asilimia 22.1 ya Pato la Taifa. Ongezeko hili linatoka na: Mahitaji ya Mfuko Mkuu wa Serikali ikijumuisha ulipaji wa deni la Serikali; Ongezeko la mahitaji ya upandishwaji wa madaraja ya watumishi na ajira mpya; na Mahitaji ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanzania National Parks Authority - TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Area Authority - NCAA). Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 4.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 40,207.4 mwaka 2023/24.

**Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Makadirio ya Matumizi**

Shilingi bilioni




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

106. Katika mwaka 2021/22, matumizi ya kawaida yanakadiriwa kukua kwa asilimia 4.1 hadi shilingi bilioni 23,003.0 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 22,100.5 mwaka 2020/21, sawa na asilimia 14.0 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, gharama za

kuhudumia Deni la Serikali ikijumuisha gharama nyingine za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 10,663.3 mwaka 2021/22 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 10,376.8 mwaka 2020/21 na Mishahara kwa Watumishi wa Umma inakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 8,150.5 mwaka 2021/22 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 7,762.4 mwaka 2020/21. Matumizi Mengineyo yanatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.5 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 4,189.2 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 4,913.9 mwaka 2023/24.

107. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuongezeka kutoka makadirio ya shilingi bilioni 12,779.3 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 13,255.9 mwaka 2021/22, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote na asilimia 8.1 ya Pato la Taifa. Makadirio ya matumizi ya maendeleo yamezingatia kukamilika kwa miradi mbalimbali kama vile maboma ya shule na vituo vya kutolea huduma za afya ambayo yanahitaji fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya uendeshaji. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 14,937.0 mwaka 2023/24. Mgawanyo wa matumizi ya kawaida na maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.4.**

**Kielelezo Na. 3.4 Makadirio ya Aina Kuu za Matumizi**

Shilingi Bilioni




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

### 3.5.3 Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi[1]

108. Mchanganuo wa matumizi ya Serikali kiuchumi hujumuisha: mishahara na stahili za watumishi; bidhaa na huduma; ruzuku kwa Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa; malipo ya riba; malipo ya mtaji wa deni; na uwekezaji/maendeleo.

109. Matumizi ya mishahara na stahili za watumishi yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 9,964.5 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 10,401.6 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 11,679.2 mwaka 2023/24. Matumizi kwenye eneo la Bidhaa na Huduma yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 4,345.0 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 4,535.6 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 5,092.7 mwaka 2023/24. Matumizi ya Ruzuku kwa Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 881.5 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 920.1 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 1,033.2 mwaka 2023/24.

110. Katika muda wa kati, malipo ya riba yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 2,870.6 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 2,713.0 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 3,319.8 mwaka 2023/24. Malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 5,779.4 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 6,165.4 mwaka 2021/22 na kupungua kufikia shilingi bilioni 6,144.1 mwaka 2023/24. Aidha, matumizi kwenye shughuli za uwekezaji/maendeleo yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 11,038.8 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 11,523.0 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 12,938.4 mwaka 2023/24. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.5.**

[1] Matumizi ya Serikali Kiuchumi (Economic Classification of expenditure) ni mgawanyo wa matumizi kufuatana na viwango vya kimataifa vinavyotolewa na mwongozo wa Shirika la Fedha la Kimataifa (GFSManual 2014).

**Kielelezo Na.3.5: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi**




***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

### 3.5.4 Makadirio ya Matumizi Kisekta

111. Matumizi kisekta yanajumuisha makadirio ya matumizi kwa kuzingatia majukumu na shughuli za Serikali. Matumizi haya yamegawanyika katika sekta za: Huduma za Utawala na Deni la Serikali; Maendeleo ya Uchumi; Elimu; Ulinzi, Utii wa Sheria na Usalama; Afya; Hifadhi ya Jamii; na Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii.

112. Katika muda wa kati, matumizi kisekta yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.9 kwa mchanganuo ufuatao; makadirio ya matumizi katika sekta ya Huduma za Utawala na Deni la Serikali yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 13,543.1 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 14,078.6 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 15,611.7 mwaka 2023/24. Aidha, makadirio ya matumizi katika sekta ya Maendeleo ya Uchumi yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 8,276.8 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 8,604.1 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 9,541.0 mwaka 2023/24. Vilevile, matumizi katika Sekta ya Elimu inakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 4,721.7 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 4,908.4 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 5,442.9 mwaka 2023/24.

113. Matumizi katika sekta ya Ulinzi, Utii wa Sheria na Usalama yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 3,302.7 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 3,433.3 mwaka 2021/22 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 3,807.2 mwaka 2023/24; matumizi katika sekta ya Afya yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,916.3 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 1,992.1 mwaka 2021/22 na

kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,209.0 mwaka 2023/24. Matumizi katika sekta ya Hifadhi ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,845.7 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 1,918.6 mwaka 2021/22 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,127.6 mwaka 2023/24. Matumizi katika sekta ya Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,273.5 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 1,323.8 mwaka 2021/22 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 1,468.0 mwaka 2023/24. Mgawanyo wa makadirio kwa kila Sekta umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3.6.**

**Kielelezo Na. 3.6: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kisekta**

Shilingi bilioni




***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

### 3.6 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati

114. Katika kuhakikisha rasilimali fedha zinazokidhi utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinapatikana, Serikali itaendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (*Development Co-operation Framework-DCF*) katika ngazi zote kama mkakati wa kuwashirikisha Washirika wa Maendeleo katika kupanga na kutekeleza programu na miradi ya kipaumbele. Utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano utasaidia kuimarisha mahusiano kati ya Tanzania na nchi rafiki pamoja na Mashirika ya Kimataifa na hivyo kuhakikisha rasilimali fedha zinapatikana kwa wakati.

115. Misaada ya Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 1,127.2 mwaka 2021/22 na kuendelea kupungua hadi shilingi bilioni 865.4 mwaka 2023/24. Misaada kupitia Mifuko ya Pamoja ya Kisekta inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 222.6

mwaka 2021/22 na kupungua hadi shilingi bilioni 218.9 mwaka 2023/24. Aidha, misaada ya miradi ya maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 904.6 mwaka 2021/22 na kuendelea kupungua hadi shilingi bilioni 646.5 mwaka 2023/24. Aidha, kwa mwaka 2021/22 hakutakuwa na Misaada ya Kibajeti kupitia utaratibu wa *General Budget Support* (GBS) kutokana na kufika ukomo wa Mkataba wa Programu ya GBS katika sekta ya Fedha na Uchumi kutoka Jumuiya ya Ulaya iliyojumuisha nchi za Denmark na Sweden.

### 3.7 Mkakati wa Kugharamia Nakisi ya Bajeti

116. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kukopa kwa gharama nafuu kadiri itakavyowezekana kutoka vyanzo vya ndani na nje ili kutoathiri uhimilivu wa Deni la Serikali. Ukopaji katika vyanzo vya ndani utalenga kugharamia bajeti pamoja na kusaidia kuendeleza soko la ndani la hatifungani. Kiasi kikubwa cha mikopo kutoka vyanzo vya nje kitakopwa kutoka Taasisi za Fedha za Kimataifa na Wakala wa Mikopo wa Kimataifa wanaotoa mikopo kwa utaratibu wa *Export Credit Agencies* kama itakavyoainishwa katika Mkakati wa kipindi cha Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali (2020/21 – 2023/24). Aidha, kutokana na uhitaji mkubwa wa kugharamia miradi ya maendeleo, Serikali italazimika kutafuta fedha kupitia mikopo yenye masharti ya kibiashara kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje.

#### 3.7.1 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani

117. Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani la dhamana za Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo bila kuathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea na jitihada za kukuza na kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali na kutekeleza hatua mbalimbali za kisera ikiwa ni pamoja na: kuboresha miundombinu ya soko kwa kuwawezesha wananchi kushiriki katika minada kwa njia ya simu za mkononi; kuongeza wastani wa muda wa uivaji wa hatifungani za Serikali ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza katika kulipa madeni kwa utaratibu wa kukopa na kurejesha mikopo iliyoiva; na kutoa elimu kwa umma ili kupanua wigo wa wawekezaji.

118. Serikali itakamilisha uanzishwaji wa Programu ya Hatifungani Kizio (*Benchmark Bond*) kwa lengo la kuongeza ujazi wa hatifungani na kuvutia wawekezaji zaidi na kuwezesha soko kuwa na viwango vya riba rejea ambavyo vitachochea ukuaji wa soko la mitaji. Katika mwaka 2021/22, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 4,989.1. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,150.3 ni kwa ajili ya kulipia mikopo itakayoiva na shilingi bilioni 1,838.8 (sawa na asilimia 1.1 ya Pato la Taifa) ni kwa ajili ya kugharamia

miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani kwa kiwango kisichozidi asilimia 1.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka ili kutoathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

### 3.7.2 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje

119. Katika mwaka 2021/22, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 4,109.9, kati ya hizo, mikopo yenye masharti nafuu ni shilingi bilioni 1,757.8 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ni shilingi bilioni 2,352.1. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 3,914.0 kwa mwaka. Mchanganuo wa Vyanzo vya Mapato katika kipindi cha muda wa kati ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.7**.

**Kielelezo Na. 3.7: Mchanganuo wa Vyanzo vya Mapato Katika Muda wa Kati**




***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

## 3.8 Vipaumbele katika Muda wa Kati

120. Katika muda wa kati, Serikali itatekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Utekelezaji wa Mpango

wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 utakuwa ni wa kwanza katika kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya Mpango huu. Aidha, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22 utajumuisha ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Baadhi ya miradi hiyo ni: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge); Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli kiwango cha standard gauge kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga; Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222); Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu (Interchange) za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na Ununuzi wa Meli za Uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay Kaskazini; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; kuendeleza Kanda Maalum za Kiuchumi; na Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii.

121. **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi:** Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika: kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana katika nyanja za ajira; kuimarisha utulivu wa uchumi; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege.

122. **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma:** Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini. Aidha, eneo hili linajumuisha pia miradi na programu inayolenga kuboresha sekta ya utalii, huduma za fedha na bima.

123. **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Eneo hili linajumuisha programu zitakazo imarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko kikanda na kimatiafa. Aidha, masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwemo bidhaa zitokanazo na kilimo na viwanda.

124. **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linajumuisha utekekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwemo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote; afya, ustawi na maendeleo ya jamii; kinga ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, na nyumba na maendeleo ya makazi.

125. **Kuendeleza Rasilimali Watu:** Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi wa rasimali watu nchini kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

### 3.9 Makadirio ya Bajeti

126. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti katika muda wa kati umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 3.1** hadi **3.5**.

**Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati**

Shilingi Milioni

| | 2020/21 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2021/22 MAKADIRIO YA BAJETI | 2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI | 2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)** | **24,065,543** | **26,032,576** | **28,214,919** | **30,852,142** |
| **Mapato ya Ndani** | **23,250,582** | **25,168,718** | **27,297,897** | **29,876,585** |
| Mapato ya TRA ( Kodi na Yasiyo ya Kodi) | 20,325,780 | 22,097,676 | 24,104,998 | 26,269,832 |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Mashirika na Taasisi) | 2,924,802 | 3,071,042 | 3,192,899 | 3,606,752 |
| **Mapato ya Halmashauri** | **814,961** | **863,858** | **917,022** | **975,558** |
| | | | | |
| **Jumla ya Matumizi** | **29,100,434** | **30,093,400** | **32,054,957** | **34,063,266** |
| Matumizi ya Kawaida | 16,321,179 | 16,837,545 | 18,030,963 | 19,126,272 |
| Malipo ya Riba Nje | 1,239,914 | 1,151,376 | 1,353,696 | 1,414,840 |
| Malipo ya Riba Ndani | 1,630,669 | 1,561,637 | 1,754,142 | 1,904,998 |
| Mishahara (Serikali Kuu na Taasisi) | 7,762,389 | 8,150,509 | 8,558,034 | 8,985,936 |
| Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 1,199,181 | 1,247,149 | 1,297,035 | 1,348,916 |
| Bidhaa/Huduma/Ruzuku | **4,489,026** | **4,726,874** | **5,068,056** | **5,471,582** |
| o/w Mataumizi Mengineyo | **3,193,765** | **3,020,850** | **3,320,133** | **3,678,538** |
| | | | | |
| Matumizi ya Maendeleo | **12,779,255** | **13,255,855** | **14,023,994** | **14,936,994** |
| Fedha za Ndani | 10,043,206 | 10,370,865 | 11,408,312 | 12,459,472 |
| Fedha za Nje | 2,736,049 | 2,884,990 | 2,615,682 | 2,477,522 |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila kujumuisha Misaada** | **-5,034,891** | **-4,060,824** | **-3,840,038** | **-3,211,124** |
| | | | | |
| **Misaada** | **949,322** | **1,127,188** | **959,108** | **865,416** |
| Misaada ya Kibajeti | 138,323 | 0 | 0 | 0 |
| Misaada ya Miradi ya Maendeleo | 614,461 | 904,618 | 733,866 | 646,543 |
| Misaada ya Mifuko ya Kisekta | 196,538 | 222,570 | 225,242 | 218,873 |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada** | **-4,085,568** | **-2,933,636** | **-2,880,930** | **-2,345,708** |
| | | | | |
| **Kuziba Nakisi** | **-4,085,568** | **-2,933,636** | **-2,880,930** | **-2,345,708** |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Nje** | **2,497,399** | **1,094,839** | **1,097,745** | **429,783** |
| Mikopo ya Kibajeti | 0 | 0 | 50,000 | 51,000 |
| Mikopo ya Miradi ya Maendeleo | 1,846,045 | 1,698,066 | 1,595,046 | 1,549,347 |
| Mikopo ya Mifuko ya Kisekta | 79,005 | 59,736 | 61,528 | 62,759 |
| Mikopo ya Kibiashara (Nje) | 3,035,630 | 2,352,107 | 2,421,900 | 1,840,650 |
| Malipo ya Mtaji Deni la Nje | -2,463,281 | -3,015,070 | -3,030,729 | -3,073,973 |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Ndani** | **1,588,169** | **1,838,796** | **1,783,185** | **1,915,925** |
| Mikopo ya Kibiashara (Ndani) | 1,588,169 | 1,838,796 | 1,783,185 | 1,915,925 |
| Mikopo ya Mtaji Deni la Ndani | 3,316,078 | 3,150,337 | 3,050,728 | 3,070,117 |
| Malipo ya Mtaji Deni la Ndani | -3,316,078 | -3,150,337 | -3,050,728 | -3,070,117 |
| ***Pato la Taifa*** | **157,767,884** | **163,879,616** | **174,534,634** | **185,936,799** |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

**Jedwali Na. 3.2 Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa Katika Muda wa Kati**

| | 2020/21 BAJETI ILIYOIDHINISHWA | 2021/22 MAKADIRIO YA BAJETI | 2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI | 2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)** | 15.3% | 15.9% | 16.2% | 16.6% |
| **Mapato ya Ndani** | 14.7% | 15.4% | 15.6% | 16.1% |
| Mapato ya TRA ( Kodi na Yasiyo ya Kodi) | 12.9% | 13.5% | 13.8% | 14.1% |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Mashirika na Taasisi) | 1.9% | 1.9% | 1.8% | 1.9% |
| **Mapato ya Halmashauri** | 0.5% | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| | | | | |
| **Jumla ya Matumizi** | 18.4% | 18.4% | 18.4% | 18.3% |
| Matumizi ya Kawaida | 10.3% | 10.3% | 10.3% | 10.3% |
| Malipo ya Riba Nje | 0.8% | 0.7% | 0.8% | 0.8% |
| Malipo ya Riba Ndani | 1.0% | 1.0% | 1.0% | 1.0% |
| Mishahara (Serikali Kuu na Taasisi) | 4.9% | 5.0% | 4.9% | 4.8% |
| Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 0.8% | 0.8% | 0.7% | 0.7% |
| Bidhaa/Huduma/Ruzuku | 2.8% | 2.9% | 2.9% | 2.9% |
| o/w Mataumizi Mengineyo | 2.0% | 1.8% | 1.9% | 2.0% |
| | | | | |
| Matumizi ya Maendeleo | 8.1% | 8.1% | 8.0% | 8.0% |
| Fedha za Ndani | 6.4% | 6.3% | 6.5% | 6.7% |
| Fedha za Nje | 1.7% | 1.8% | 1.5% | 1.3% |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti bila kujumuisha Misaada** | -3.2% | -2.5% | -2.2% | -1.7% |
| | | | | |
| **Misaada** | 0.6% | 0.7% | 0.5% | 0.5% |
| Misaada ya Kibajeti | 0.1% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Misaada ya Miradi ya Maendeleo | 0.4% | 0.6% | 0.4% | 0.3% |
| Misaada ya Mifuko ya Kisekta | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.1% |
| | | | | |
| **Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada** | -2.6% | -1.8% | -1.7% | -1.3% |
| | | | | |
| **Kuziba Nakisi** | -2.6% | -1.8% | -1.7% | -1.3% |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Nje** | 1.6% | 0.7% | 0.6% | 0.2% |
| Mikopo ya Kibajeti | 0.0% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Mikopo ya Miradi ya Maendeleo | 1.2% | 1.0% | 0.9% | 0.8% |
| Mikopo ya Mifuko ya Kisekta | 0.1% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Mikopo ya Kibiashara (Nje) | 1.9% | 1.4% | 1.4% | 1.0% |
| Malipo ya Mtaji Deni la Nje | -1.6% | -1.8% | -1.7% | -1.7% |
| **Kuziba Nakisi Kutoka Ndani** | 1.0% | 1.1% | 1.0% | 1.0% |
| Mikopo ya Kibiashara (Ndani) | 1.0% | 1.1% | 1.0% | 1.0% |
| Malipo ya Mtaji Deni la Ndani | 2.1% | 1.9% | 1.7% | 1.7% |
| Malipo ya Mtaji Deni la Ndani | -2.1% | -1.9% | -1.7% | -1.7% |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

**Jedwali Na.3.3: Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati**

Shilingi Milioni

| | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI |
| | | | | |
| **I. JUMLA YA MAPATO** | **34,879,793** | **36,258,806** | **38,136,414** | **40,207,356** |
| | | | | |
| Mapato ya Ndani | 23,250,582 | 25,168,718 | 27,297,897 | 29,876,585 |
| Mapato ya Halmashauri | 814,961 | 863,858 | 917,022 | 975,558 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 138,323 | 0 | 50,000 | 51,000 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 2,460,506 | 2,602,684 | 2,328,912 | 2,195,890 |
| Mifuko ya Kisekta | 275,543 | 282,306 | 286,770 | 281,632 |
| Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | 3,316,078 | 3,150,337 | 3,050,728 | 3,070,117 |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara | 1,588,169 | 1,838,796 | 1,783,185 | 1,915,925 |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | 3,035,630 | 2,352,107 | 2,421,900 | 1,840,650 |
| | | | | |
| **II. JUMLA YA MATUMIZI** | **34,879,793** | **36,258,806** | **38,136,414** | **40,207,356** |
| | | | | |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 22,100,538 | 23,002,951 | 24,112,420 | 25,270,362 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 10,376,832 | 10,663,278 | 11,034,039 | 11,370,553 |
| Mishahara | 7,762,389 | 8,150,509 | 8,558,034 | 8,985,936 |
| Matumizi Mengineyo | 3,961,316 | 4,189,164 | 4,520,346 | 4,913,873 |
| | | | | |
| MATUMIZI YA MAENDELEO | 12,779,255 | 13,255,855 | 14,023,994 | 14,936,994 |
| | | | | |
| Fedha za Ndani | 10,043,206 | 10,370,865 | 11,408,312 | 12,459,472 |
| Fedha za Nje | 2,736,049 | 2,884,990 | 2,615,682 | 2,477,522 |
| ***GDPmp*** | **157,767,884** | **163,879,616** | **174,534,634** | **185,936,799** |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

**Jedwali Na. 3.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa katika Muda wa Kati**

| | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI |
| | | | | |
| **I. JUMLA YA MAPATO** | **22.1%** | **22.1%** | **21.9%** | **21.6%** |
| | | | | |
| Mapato ya Ndani | 14.7% | 15.4% | 15.6% | 16.1% |
| Mapato ya Halmashauri | 0.5% | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 0.1% | 0.0% | 0.0% | 0.0% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 1.6% | 1.6% | 1.3% | 1.2% |
| Mifuko ya Kisekta | 0.2% | 0.2% | 0.2% | 0.2% |
| Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | 2.1% | 1.9% | 1.7% | 1.7% |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara | 1.0% | 1.1% | 1.0% | 1.0% |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | 1.9% | 1.4% | 1.4% | 1.0% |
| | | | | |
| **II. JUMLA YA MATUMIZI** | **22.1%** | **22.1%** | **21.9%** | **21.6%** |
| | | | | |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 14.0% | 14.0% | 13.8% | 13.6% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 6.6% | 6.5% | 6.3% | 6.1% |
| Mishahara | 4.9% | 5.0% | 4.9% | 4.8% |
| Matumizi Mengineyo | 2.5% | 2.6% | 2.6% | 2.6% |
| | | | | |
| MATUMIZI YA MAENDELEO | 8.1% | 8.1% | 8.0% | 8.0% |
| | | | | |
| Fedha za Ndani | 6.4% | 6.3% | 6.5% | 6.7% |
| Fedha za Nje | **1.7%** | **1.8%** | **1.5%** | **1.3%** |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

**Jedwali Na. 3.5: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Bajeti Yote katika Muda wa Kati**

| | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI | MAKADIRIO YA BAJETI |
| | | | | |
| **I. JUMLA YA MAPATO** | **100%** | **100%** | **100%** | **100%** |
| | | | | |
| Mapato ya Ndani | 66.7% | 69.4% | 71.6% | 74.3% |
| Mapato ya Halmashauri | 2.3% | 2.4% | 2.4% | 2.4% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 0.4% | 0.0% | 0.1% | 0.1% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 7.1% | 7.2% | 6.1% | 5.5% |
| Mifuko ya Kisekta | 0.8% | 0.8% | 0.8% | 0.7% |
| Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | 9.5% | 8.7% | 8.0% | 7.6% |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara | 4.6% | 5.1% | 4.7% | 4.8% |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | 8.7% | 6.5% | 6.4% | 4.6% |
| | | | | |
| **II. JUMLA YA MATUMIZI** | **100%** | **100%** | **100%** | **100%** |
| | | | | |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | **63.4%** | **63.4%** | **63.2%** | **62.9%** |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 29.8% | 29.4% | 28.9% | 28.3% |
| Mishahara | 22.3% | 22.5% | 22.4% | 22.3% |
| Matumizi Mengineyo | 11.4% | 11.6% | 11.9% | 12.2% |
| | | | | |
| MATUMIZI YA MAENDELEO | **36.6%** | **36.6%** | **36.8%** | **37.1%** |
| | | | | |
| Fedha za Ndani | 28.8% | 28.6% | 29.9% | 31.0% |
| Fedha za Nje | **7.8%** | **8.0%** | **6.9%** | **6.2%** |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

# SURA YA NNE

## USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA BAJETI

### 4.1. Utangulizi

127. Sura hii inabainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti pamoja na hatua za kukabiliana na vihatarishi hivyo kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu Na. 4 (2) (c) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439.

### 4.2. Vihatarishi vya Uchumi na Bajeti

128. Vihatarishi vinavyoweza kusababisha madhara katika ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa bajeti ni pamoja na:

129. **Mabadiliko ya Bei za Bidhaa:** kupanda kwa bei za bidhaa katika masoko ya ndani na nje husababisha ongezeko la gharama za upatikanaji wa bidhaa muhimu zikiwemo bidhaa za petroli, pembejeo za kilimo, malighafi za viwandani na vifaa vya ujenzi na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukuaji katika shughuli za kiuchumi. Aidha, kushuka kwa bei za bidhaa katika masoko ya nje kutaathiri upatikanaji wa mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

130. **Mabadiliko ya Viwango vya Kubadilisha Fedha:** kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni kunaweza kusababisha ongezeko la gharama za uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukuaji wa uchumi. Aidha, kwa kuwa sehemu kubwa ya deni la Serikali ni mikopo kutoka nje, kushuka kwa thamani ya shilingi kutaongeza gharama za ulipaji wa deni na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

131. **Mabadiliko ya Viwango vya Riba:** kupanda kwa viwango vya riba za mikopo kusikotarajiwa katika masoko ya fedha ya ndani na nje kutasababisha ongezeko la matumizi ya malipo ya riba na nakisi ya bajeti. Aidha, mikopo ya ndani hulipwa kwa utaratibu wa kuzungusha mtaji, hivyo endapo Serikali itashindwa kukopa kutokana na ongezeko la riba au wawekezaji wa ndani kushindwa kukopesha kwa kiwango kinachotakiwa, Serikali italazimika kutumia mapato kutoka vyanzo vingine kugharamia mikopo iliyoiva. Vilevile, mabadiliko yasiyotarajiwa ya viwango vya riba katika benki na taasisi za fedha husababisha sekta binafsi kutofikia malengo ya mikopo na hivyo kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusababisha Serikali kukosa mapato.

132. **Madeni Sanjari kutokana na Dhamana za Serikali:** utoaji wa dhamana za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ni miongoni mwa maeneo yanayoweza kuwa na athari katika utekelezaji wa bajeti endapo hakutakuwa na usimamizi madhubuti. Serikali imekuwa ikitoa dhamana kwa Mashirika na Taasisi ili kuziwezesha kukopa ndani. Aidha, Serikali hukopa mikopo ya gharama nafuu kutoka nje na kuyakopesha Mashirika na Taasisi kwa lengo la kuyapunguzia gharama ya riba na uendeshaji. Utoaji wa dhamana unaweza kusababisha madeni sanjari kwa Serikali endapo Mashirika na Taasisi zilizopatiwa dhamana zitashindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa. Vile vile, madeni sanjari huongeza mzigo wa madeni kwa Serikali na hivyo kusababisha Serikali kutumia mapato ambayo yangetumika kugharamia huduma za jamii na shughuli za uzalishaji kulipa madeni husika.

133. **Madeni Sanjari kutokana na Madai na Mashauri ya Kisheria Dhidi ya Serikali:** Madai na mashauri ya kisheria yasiyotarajiwa dhidi ya Serikali ni miongoni mwa maeneo yanayoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti endapo mahakama itatoa maamuzi ya kushindwa kwa Serikali katika mashauri husika. Hali hiyo itailazimu Serikali kutumia fedha za bajeti zilizotengwa kutekeleza shughuli nyingine ili kutekeleza uamuzi wa mahakama na hivyo kuathiri malengo ya bajeti.

134. **Ajali na Upotevu wa Mali**: Ajali na upotevu wa mali kutokana na udanganyifu, wizi na majanga huathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kuongeza mahitaji ya matumizi ya bajeti iliyotengwa. Hali hii husababisha matumizi ya ziada na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwenye bajeti ya Serikali.

135. **Kutopatikana Misaada na Mikopo kwa Wakati**: Misaada na mikopo ni mojawapo ya vyanzo vya mapato ya Serikali. Mwenendo usioridhisha wa masoko ya fedha ndani na nje husababisha Serikali kukosa kiasi cha mikopo iliyopangwa kukopwa katika mwaka husika. Aidha, Washirika wa Maendeleo wasipotimiza ahadi ya misaada iliyotengwa kwenye bajeti husababisha upungufu katika mapato ya Serikali na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti.

136. **Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga ya Asili:** mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili ni miongoni mwa vihatarishi vinavyoathiri utekelezaji wa mipango na bajeti. Majanga hayo ni pamoja na ukame, mafuriko, matetemeko, maporomoko ya ardhi, na magonjwa ya mlipuko, mathalan *COVID-19*. Kutokea kwa majanga hayo huathiri shughuli za kiuchumi zikiwemo kupungua kwa uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa na huduma. Aidha, uharibifu wa miundombinu unaweza kusababisha athari nyingine kwenye uchumi zikiwemo: kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani; kuongezeka kwa mfumuko wa bei; kupungua kwa faida za

kampuni na hivyo kusababisha upungufu katika ukusanyaji wa mapato na kuongezeka kwa nakisi ya bajeti.

### 4.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

137. Hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na vihatarishi ni pamoja na:

(i) **Mabadiliko ya Bei za Bidhaa:** kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani kwa kujenga viwanda vya kuzalisha pembejeo za kilimo na bidhaa nyingine muhimu ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje, kuongeza akiba ya mafuta ya petroli na kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani ili kuongeza ushindani katika masoko ya nje.

(ii) **Mabadiliko ya Viwango vya Kubadilisha Fedha:** kuendelea kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Fedha ikiwemo kudhibiti ujazi wa fedha, kudhibiti mzunguko wa fedha haramu na kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

(iii) **Mabadiliko ya Viwango vya Riba:** kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi ili kupunguza utegemezi katika misaada na mikopo. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza Sera zitakazowezesha viwango vya riba kuwa himilivu ili kuchochea uwekezaji.

(iv) **Madeni Sanjari kutokana na Dhamana za Serikali:** kuendelea kusimamia dhamana zilizotolewa na kudhibiti utoaji wa dhamana za Serikali kwa Mashirika na Taasisi mbalimbali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

(v) **Madeni Sanjari kutokana na Madai na Mashauri ya Kisheria Dhidi ya Serikali:** kuendelea kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo katika usimamizi wa mikataba ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali pamoja na kuhimiza wataalamu wa Serikali kuzingatia weledi katika usimamizi na utekelezaji wa sheria.

(vi) **Ajali na Upotevu wa Mali**: kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uwepo wa huduma na vifaa vya kudhibiti majanga na kuendelea kuhimiza watumishi wa umma kuzingatia maadili na weledi katika usimamizi na utunzaji wa mali za umma.

(vii) **Kutopatikana Misaada na Mikopo kwa Wakati**: kuhakikisha deni linabaki kuwa himilivu na kuelekeza mikopo kwenye miradi inayochochea shughuli za uzalishaji. Vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo pamoja na kuhimiza Washirika wa Maendeleo kutoa misaada waliyoahidi kwa wakati.

(viii) **Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga ya Asili:** kuendelea kutekeleza Muundo wa Usimamizi wa Maafa unaoelekeza utaratibu wa kupunguza athari za majanga; kuhakikisha Kamati ya Maafa ya Kitaifa pamoja na za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinaandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya kuepusha na kukabiliana na maafa

yanayotokana na majanga ya asili; kuendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya teknolojia katika kutekeleza shughuli za maendeleo ili kupunguza athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira; na kuendelea kuimarisha mifumo ya kubainisha maeneo hatarishi, kutabiri majanga na kuchukua tahadhari pamoja na kutekeleza miradi inayohimili athari za majanga ya asili.

(ix) Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa Serikali kuhusu Mwongozo wa Uandaaji wa Muundo wa Usimamizi wa Vihatarishi unaoelekeza namna ya kubainisha vihatarishi; hatua za kukabiliana na vihatarishi; na uanzishaji wa Daftari la Orodha ya Vihatarishi *(Risk Register)*.

## SEHEMU YA PILI

## MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

# SURA YA KWANZA

# MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

## 1.1. Uandaaji wa Mpango na Bajeti

138. Wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia vipaumbele vya Sera na Miongozo iliyorejewa katika Mwongozo huu wa Mwaka 2021/22, pamoja na Mpango Mkakati wa taasisi husika. Aidha, wanapaswa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21 na kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa changamoto zilizobainishwa katika Mwongozo wa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kutoshirikisha kikamilifu Kamati za Bajeti za Mafungu katika uandaaji na utekelezaji wa bajeti; kutowasilishwa kwa wakati kwa taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji wa bajeti kwa baadhi ya Mafungu; na baadhi ya Mafungu kuendelea kuwasilisha mahitaji ya fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

139. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya mipango ya maendeleo na shughuli muhimu za uendeshaji wa ofisi ikiwemo umeme, maji, simu, ulinzi na usafi, pamoja na kulipa madeni ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni, riba na faini. Taasisi za Serikali zinazotarajia kupokea mikopo, misaada na dhamana zitapaswa kupata idhini kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha, kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

140. Wizara za Muungano zinaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

### 1.1.1. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

141. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma zinaelekezwa kuandaa Mpango na Bajeti shirikishi kwa kuzingatia Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Mawasilisho hayo yanatakiwa kufanyika wiki ya pili ya Februari 2021 baada ya kuidhinishwa katika ngazi za maamuzi husika ikihusisha Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura 105. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwasilisha MTEF Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina wiki ya kwanza ya Februari 2021.

### 1.1.2. Kamati za Bajeti

142. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuunda Kamati za Bajeti kwa kuzingatia Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 17 (2) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015. Aidha, Kamati za Bajeti zinapaswa kushiriki kikamilifu wakati wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ili kuwepo kwa mipango na utekelezaji shirikishi katika Mafungu kama ilivyobainishwa katika Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015. Vilevile, taarifa ya utekelezaji wa Kamati za Bajeti kuhusu maandalizi na ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi wakati wa utekelezaji wa bajeti ijumuishwe katika Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

### 1.1.3. Maandalizi ya Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

143. Wakati wa kuandaa bajeti ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2021/22, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutambua na kutenganisha vyanzo vyote vya mapato katika makundi ya vyanzo lindwa (protected sources) na visivyolindwa (unprotected sources);
(ii) Kutenga angalau asilimia 40 ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo;
(iii) Kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa uwiano wa asilimia nne, nne na mbili kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (37A) na Kanuni zake za Mwaka 2019;
(iv) Kutojumuisha michango ya nguvu za wananchi kwenye bajeti ya vyanzo vya mapato ya ndani;
(v) Kushirikisha Kamati ya Bajeti na wadau wengine kulingana na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kupitisha kwenye vikao vya kisheria, na kuushirikisha Mkoa kabla ya kuwasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na
(vi) Halmashauri zinazopokea mapato mengine kama vile michango ya kijamii (Corporate Social Responsibility) na wadau wa maendeleo wahakikishe wanajumuisha mapato hayo kwenye bajeti zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

### 1.1.4. Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara

144. Wakati wa kuandaa ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka 2021/22, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuhakikisha maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo upandishaji vyeo unazingatia bajeti, ikama na Miundo ya Maendeleo ya Utumishi na Kanuni D.51 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009;
(ii) Kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 2015 na

Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 6 wa Mwaka 2015 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa watumishi wa Umma na Taasisi za Serikali;

(iii) Kujumuisha makisio ya nyongeza za mwaka za mishahara na upandishwaji vyeo katika bajeti ya mishahara kwa mwaka 2021/22;

(iv) Kuzingatia Mwongozo wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) kuhusu uandaaji wa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa Mwaka 2021/22; na

(v) Kuzingatia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu (2008), pamoja na masuala ya Jinsia, VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa.

## 1.2. Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti

### (a) Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo

145. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo *(NPMIS)* katika kuandaa na kutekeleza miradi ya maendeleo na kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2020/21 kuhusu Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo;

(ii) Kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na Upokeaji wa Misaada wa mwaka 2020 (Guidelines for Project Planning and Negotiations for Raising Loans, Issuing Guarantees and Receiving Grants 2020);

(iii) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 6 wa mwaka 2020 unaoelezea Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Msamaha wa Kodi ya Ongozeko la Thamani (VAT) katika Ununuzi wa Bidhaa au Huduma Katika Miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali na za Washirika wa Maendeleo na kutumia Mfumo wa Kieletroniki wa Kutunza Taarifa za Msamaha wa Kodi (Tax Exemption System) kila wanapoomba msamaha wa kodi kwa miradi yote inayohusisha msamaha wa kodi;

(iv) Kuhakikisha misamaha ya kodi iliyotolewa katika miradi ya maendeleo inatumika ipasavyo ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha hiyo;

(v) Wizara za Kisekta zinazoratibu miradi na programu zinazoshirikisha utekelezaji wa Mafungu mengine kuhakikisha bajeti ya shughuli zinazohusu Mafungu hayo inatengwa kwenye Mafungu husika;

(vi) Kuzingatia Mwongozo wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kutekeleza awamu ya pili ya kuhamia Dodoma;

(vii) Kuomba idhini ya kuvusha matumizi ya fedha kwa mwaka unaofuata kabla ya tarehe 15 Juni kila mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015; na

(viii) Kutumia fedha za miradi zilizovuka mwaka wa fedha (2020/21) kabla ya Septemba 30, 2021. Endapo kutakuwa na sababu za msingi za kutotumia fedha hizo, kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali kiombwe kuongeza muda wa matumizi kwa mujibu wa Kanuni ya 2 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015 na marekebisho ya Mwaka 2019.

**(b) Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato**

146. Katika mwaka 2021/22, Serikali itatoa kipaumbele katika ukamilishaji wa miradi ya kimkakati. Maafisa Masuuli wanaotekeleza miradi ya kimkakati wanaelekezwa kutenga bajeti husika na kuendelea kusimamia kikamilifu miradi hiyo ili kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na kuzingatia thamani ya fedha.

**(c) Ugharamiaji wa Miradi Kupitia Fedha za Nje**

147. Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaendelea kutekeleza na kugharamia programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo. Hivyo, katika kuandaa bajeti ya miradi inayogharamiwa na fedha za nje, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutoingia Mikataba ya Makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134;

(ii) Kuwasilisha ukomo wa bajeti za kisekta Wizara ya Fedha na Mipango (kwa Wizara zinazoratibu Mifuko ya Pamoja ya Kisekta) kabla ya tarehe 31 Januari 2021;

(iii) Kuwasilisha takwimu za ahadi za fedha za nje Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya kwanza ya Februari 2021 ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za Mafungu; na

(iv) Kutenga *counterpart fund* katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo.

**(d) Usimamizi wa Fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D – Fund)**

148. Katika usimamizi wa fedha za Misaada au Mikopo zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo moja kwa moja katika Mafungu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo (*D- Fund*), Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia: maelekezo ya Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 unaoelekeza utaratibu wa kuomba, kuhamisha, kupokea, kutumia, kuhasibu na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zinazotumia fedha za mikopo au misaada inayopelekwa moja kwa moja kwenye Mafungu; na matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha Zinazopelekwa Moja kwa Moja kwenye Miradi (*D – Fund Management Information System*).

**(e) Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi**

149. Maafisa Masuuli wa Taasisi za Umma zinazokusudia kutekeleza miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi kama njia mbadala ya kugharamia miradi ya maendeleo zinaelekezwa kuzingatia: Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 na Kanuni za Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi za mwaka 2020, Kifungu cha 7 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinachohusu kujumuisha miradi ya PPP katika bajeti; pamoja na kipengele 3.1.2 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma *(Public Investment Management - Operational Manual*).

**(f) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu**

150. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kutenga bajeti ya kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) na kuimarisha utawala bora pamoja na kuhuisha nyenzo muhimu za utekelezaji wa Mkakati hususan mkataba wa Huduma kwa Wateja na Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko.

**(g) Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**

151. Katika kutekeleza Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu (PSRP III), Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya: kuwajengea uwezo viongozi na watumishi wa ngazi zote Serikalini; kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya maendeleo, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Serikali; kufanya utafiti kabla ya kuandaa au kuhuisha sera na mipango; kuweka misingi itakayoimarisha uwajibikaji; na kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu kwa kuboresha taratibu za ajira, uteuzi, upandishaji vyeo na muda wa matazamio kwa kuzingatia sifa na vigezo.

**(h) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili**

152. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaweka msisititizo katika kilimo chenye tija, usalama wa chakula na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda na masoko. Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa kutenga fedha kwa kuzingatia maeneo makuu manne (4) ya vipaumbele kama ifuatavyo;

(i) Kusimamia kikamilifu matumizi endelevu ya maji na ardhi;
(ii) Kuongeza tija na faida kwenye kilimo, mifugo na uvuvi;
(iii) Kuimarisha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; na
(iv) Kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji wa kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

**(i) Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

153. Katika kutekeleza Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali inalenga kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuendelea kutekeleza ugatuaji wa madaraka kisiasa, kifedha, kiutawala na kuimarisha mahusiano ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;

(ii) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara za kisekta na waliopo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye maeneo ya uratibu, ufuatiliaji, tathmini, utawala bora, elimu ya uraia, usimamizi wa fedha, mpango na bajeti, uandaaji taarifa, uandaaji na usimamizi wa miradi ili kuboresha huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuweka mazingira wezeshi ya kuboresha shughuli za kiuchumi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(iv) Kuimarisha ushiriki wa jamii katika utekelezaji na utoaji wa maamuzi kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**(j) Uendelezaji wa Huduma za Fedha**

154. Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha pamoja na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwenye shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi, Serikali inaendelea kutekeleza sera, sheria na mikakati mbalimbali ili kujenga mfumo thabiti katika sekta ya fedha. Ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Fedha wa miaka kumi (2020/21 -2029/30) na kuujumuisha katika Mpango na Bajeti wa Fungu husika;

(ii) Kuhamasisha na kusisitiza matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika sekta ya fedha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma kuhusu: huduma ya fedha zilizopo nchini; masoko ya mitaji na dhamana; soko la bidhaa; na fursa zilizopo katika taasisi za fedha za maendeleo;

(iv) Kuhamasisha, kuanzisha na kuboresha vituo vya kuendeleza biashara za huduma za fedha kwa madhumuni ya kurahisisha kuvitambua kisheria, kuviwezesha na hivyo kutoa huduma bora kwa ufanisi;

(v) Kuhakikisha kuwa mpango na bajeti za Mikoa na Halmashauri inajumuisha masuala ya huduma za fedha ikiwa ni pamoja na kuhuisha sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuboresha taratibu za usajili wa hati miliki za ardhi na mali ili kuwawezesha wananchi kutumia hati miliki kama dhamana za mikopo katika benki, taasisi

za fedha, na watoa huduma ndogo za fedha. Mikopo hiyo, itawezesha kuchochea shughuli za kiuchumi na kuondoa umaskini; na

(vii) Kuwezesha upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha kwa usawa na kwa kuzingatia gharama nafuu kwa wote ikijumuisha makundi ya watu wenye mahitaji maalum, vijana na jinsia.

**(k) Usimamizi wa Mali za Umma**

155. Katika kuimarisha usimamizi wa mali za umma kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019; na Waraka wa Hazina Na.2 wa Mwaka 2018/19 kuhusu Utaratibu wa Umiliki wa Magari na Mali Zinazotumika kwenye Miradi Inayogharamiwa na Serikali na Fedha za Washirika wa Maendeleo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuandaa na kuhuisha taarifa za mali katika Daftari la Mali (*Asset Register*) kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma na hivyo kuwa na kumbukumbu sahihi za mali;

(ii) Kupima na kurasimisha maeneo yanayomilikiwa na Serikali ikijumuisha mashamba, shule/vyuo, vituo vya kutolea huduma ya afya na ofisi za taasisi za Umma pamoja na kudhibiti, usalama na ulinzi wa mali za umma;

(iii) Kuandaa na kuhuisha Mpango wa Matengenezo wa Mali (*Asset Maintenance Plan*);

(iv) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango orodha ya mali, nyaraka za umiliki na mali husika zinazotokana na miradi inayogharamiwa na Serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo baada ya miradi kukamilika na mali zilizotaifishwa au kutelekezwa; na

(v) Kutenga bajeti ya kugharamia mafunzo na kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Mali (GAMIS) kwa ajili ya kuhuisha taarifa ya mali za umma.

**(l) Mifumo ya Kielektroniki ya Ukusanyaji wa Mapato na Ulipaji Serikalini**

156. Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 pamoja na Kanuni za GePG za mwaka 2019 zinaelekeza matumizi ya Mfumo wa GePG katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha mapato yote katika Taasisi za Umma yanaendelea kukusanywa kupitia Mfumo wa GePG.

157. Maafisa Masuuli wanasisitizwa kuhakikisha Taasisi zao zinafundishwa na kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na maelekezo ya barua ya Katibu Mkuu - Hazina yenye Kumb. Na MG.4/261/01/64 ya tarehe 03 Aprili, 2020 ambayo inasisitiza matumizi ya MUSE.

**(m) Hatua za Kudhibiti Matumizi**

158. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma ili kuongeza tija na kupata thamani ya fedha. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha, Sura 348, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni zake kwa kufanya ununuzi wa pamoja na kutumia Mwongozo wa Matumizi ya *Force Account* wa Mei 2020 ili kupata thamani halisi ya fedha;

(ii) Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kwenye ununuzi wa magari baada ya kupata ushauri wa kiufundi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) na kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(iii) Taasisi za Umma zinazotoa huduma Serikalini zikiwemo TEMESA, GPSA, TBA kuhakikisha gharama za huduma wanazozitoa ni bora na zinaakisi thamani ya fedha;

(iv) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;

(v) Kutoingia mikataba bila kuwa na bajeti ili kuepuka malimbikizo ya madai kwa kuzingatia Mwongozo Kuhusu Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

(vi) Kuhakikisha gharama za miradi inayoendelea zinajumuishwa kwenye mpango na bajeti kabla ya kuanzisha miradi mipya;

(vii) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali ili kupunguza gharama;

(viii) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa Mwaka 2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika ununuzi, uandaaji na usimikaji wa mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa fedha za Umma ili kuondoa urudufu wa mifumo;

(ix) Kuendelea kutumia kumbi za Taasisi za Umma kwa semina, mafunzo, warsha na mikutano ikiwemo ya Bodi za Wakurugenzi;

(x) Kuingia mikataba na watoa huduma wa ndani kwa kutumia Shilingi ya Tanzania ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha;

(xi) Kuepuka uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi iwapo zinazalishwa na kupatikana nchini; na

(xii) Kutumia vifaa vyenye teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati.

**(n) Ulipaji na Udhibiti wa Ulimbikizaji wa Madeni**

159. Kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439 kifungu cha 52(2), pamoja na Waraka wa Hazina Na. 4 wa mwaka 2014/15; Waraka wa Hazina Na.1 wa Mwaka 2018/19; na Waraka wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2019 kuhusu Uzuiaji, Udhibiti na

Ulipaji wa Madeni ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuepuka uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni;
(ii) Kuhakikisha madeni yote yanahakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali;
(iii) Kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa; na
(iv) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Madeni (Government Arrears Management System – GAMS) pamoja na kutunza kumbukumbu na nyaraka/vielelezo vya madeni.

**(o) Kiwango cha Ubadilishaji Fedha**

160. Makadirio yote ambayo yanatumia fedha za kigeni, yatumie kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni cha Dola Moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,352.11 katika kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22.

**(p) Kujumuisha Masuala Mtambuka katika Mpango na Bajeti**

161. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mtambuka ikiwemo Watu Wenye Ulemavu, wazee, Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU), UKIMWI, Jinsia, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, na utawala bora pamoja na Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22) na Mkakati wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee (2018/19 – 2022/23). Aidha, Maafisa Masuuli watenge bajeti kwa ajili ya kujenga au kukarabati miundombinu ya majengo ili yawe rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee.

**(q) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

162. Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kutekeleza makubaliano, itifaki na mikataba iliyoridhiwa katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia masuala ya ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mashirika ya Kimataifa pamoja na masuala mengine ya mtangamano katika Mpango na Bajeti za Mafungu;
(ii) Kuainisha na kutumia fursa zinazopatikana kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kukuza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; na
(iii) Kuwasilisha taarifa za michango ya uanachama ya Kikanda na Kimataifa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujumuishwa na kutengewa bajeti.

**1.3. Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma**

163. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kuboresha utendaji na usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na tija. Katika

kufikia azma hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutumia mfumo wa kibajeti wa PlanRep kwa ajili ya usimamizi wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22;

(ii) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kutenga na kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi na asilimia 70 ya ziada ya mapato baada ya kutoa matumizi yaliyoidhinishwa;

(iii) Kuandaa na kuwasilisha Mikakati ya Uwekezaji, sera ya gawio (dividend policy) na Mipango ya Biashara katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupata idhini;

(iv) Kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanaingia Mkataba wa Utendaji Kazi pamoja na kuwasilisha utekelezaji wa Mikataba kila robo mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina;

(v) Kuhuisha taarifa za Bodi za Wakurugenzi katika Mfumo wa Usimamizi wa Bodi (OTRMIS); na

(vi) Kutumia geresho la kibajeti (GFS Code 2014) 28211124 - *Contribution to Consolidated Fund* wakati wa kuingiza takwimu za michango itakayowasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

## 1.4. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

### 1.4.1. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa

164. Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kutekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kuendelea kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo ya utawala;

(ii) Kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya Vikao vya Ushauri vya Wilaya na Mikoa pamoja na Vikao vya Kamati za Usalama za Wilaya na Mikoa;

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa katika Mikoa na Halmashauri na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto;

(iv) Kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mikoa, Wilaya na Tarafa;

(v) Kuhuisha Mipango Mikakati ya Mikoa, Wasifu wa Mikoa na Mikakati ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Mikoa ili kuendana na maelekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Mwaka 2020 hadi 2025, Vipaumbele vinavyoibuliwa kupitia Mwongozo wa Fursa na Vikwazo vya Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2023, Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI na

kuweka taarifa na takwimu zote muhimu kwenye Tovuti za Sekretarieti za Mikoa;

(vi) Kutenga fedha za ufuatiliaji na tathmini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vii) Kutenga fedha za ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ofisi na makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa. Aidha, kipaumbele ni kutekeleza miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya;

(viii) Kuingiza kwa usahihi takwimu za bajeti kwenye Mfumo wa CBMS kwa fedha za ruzuku ya uendeshaji wa kisekta katika Serikali za Mitaa kwa kutumia vifungu maalum vilivyoainishwa kwa ajili ya fedha za mishahara, matumizi mengineyo na fedha za maendeleo;

(ix) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za huduma ndogo za fedha katika ngazi ya Mkoa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017 na Mkakati wa Utekelezaji wake pamoja na Sheria ya Huduma ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018 na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 - 2029/30;

(x) Kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kubuni, kuandaa maandiko na kufuatilia utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na vyanzo vingine vya mapato ya ndani;

(xi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa Sekretarieti za Mikoa ili kutoa ushauri wa kitaalam kwa watumishi wa Serikali za Mitaa;

(xii) Kuendelea kuwekeza na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda;

(xiii) Kusimamia Programu ya Kuendeleza Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo ngazi ya Wilaya (DADPs);

(xiv) Kusimamia utekelezaji wa Kamati za Bajeti kuhusu maandalizi na ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi wakati wa utekelezaji wa bajeti na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na

(xv) Kusimamia utekelezaji wa malengo ya Programu ya Uimarishaji wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

### 1.4.2. Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

165. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Masuuli wanapaswa kutekeleza maelekezo yafuatayo:

### A. Maelekezo ya jumla

(i) Kusimamia na kudumisha masuala ya Ulinzi na Usalama;

(ii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo ya utawala kwa kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto, na kuwezesha kufanyika kwa

vikao vya kisheria vya Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji;

(iii) Kupitia, kurekebisha na kutunga Sheria Ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na Utawala Bora katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iv) Kuimarisha Kamati za Maafa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kukabiliana na majanga asilia ikijumuisha utayari, mafunzo na uwepo wa vifaa katika maeneo ya utawala;

(v) Kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa;

(vi) Kutumia Mwongozo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019 katika kuainisha vipaumbele vya maendeleo na kujumuishwa kwenye Mpango na Bajeti za Halmashauri;

(vii) Kuweka mazingira wezeshi na kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu, vijana na wanawake;

(viii) Kuainisha, kuchambua na kuwasilisha miradi kwenye Kitengo cha Ubia cha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mujibu wa Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 na Kanuni za Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta ya Binafsi za Mwaka 2020;

(ix) Kuhuisha Mipango Mikakati ya Halmashauri, Mikakati ya Maendeleo ya Kiuchumi kulingana na vipaumbele vya maeneo husika na Wasifu wa Halmashauri kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Mwaka 2020 hadi 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, na Hati ya Majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

(x) Kutekeleza Mwongozo wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa Machi, 2018 na Mpango Mkakati wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Biashara Nchini wa Mwaka 2018;

(xi) Kukuza fursa za ajira na uchumi wa maeneo husika kwa kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha;

(xii) Kuboresha Huduma Ndogo ya Fedha kwa kuanzisha Kamati za Usimamizi, kuhuisha kanzidata ya vikundi vya fedha vya kijamii, kuvisajili, kuvijengea uwezo, kuvipatia mafunzo ya ujasiriamali, kuhamasisha urasimishaji wa watoa huduma ndogo za fedha, kufanya ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa taarifa za vikundi vya fedha vya kijamii;

(xiii) Kutenga fedha kwa ajili ya marejesho ya mikopo na michango ya wanachama kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kulipa mikopo kutoka taasisi za fedha na benki;

(xiv) Kuandaa mipango na makadirio ya vituo vya kutolea huduma kama shule, vituo vya afya, zahanati na hospitali na kujumuisha kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;

(xv) Kutenga fedha za ujenzi, ukarabati na ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashauri, Ofisi za Kata na Mitaa/Vijiji. Aidha, kipaumbele ni kutekeleza miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya;

(xvi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Jimbo;

(xvii) Kutambua na kuendeleza wabunifu wa teknolojia kwa ajili ya kuwaendeleza na kuboresha huduma; na

(xviii) Kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019.

**B. Maelekezo kuhusu Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Ardhi na Mazingira.**

(i) Kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kupata utaalam na mbinu bora kutoka kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa ambao wapo kwenye maeneo yao ili kukuza uwezo na kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara;

(ii) Kuendelea kuwekeza na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda;

(iii) Kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo ngazi ya Halmashauri (DADPs);

(iv) Kutumia sehemu ya mapato ya kilimo, mifugo na uvuvi kuwawezesha Maafisa Ugani ili waweze kutoa huduma bora za ugani na kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na mamlaka za utafiti na udhibiti;

(v) Kushirikiana na Wizara za Kisekta kukamilisha ukarabati na ujenzi wa miradi inayoendelea katika Halmashauri kabla ya kuanzisha miradi mipya;

(vi) Kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika;

(vii) Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga bajeti ya uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;

(viii) Kuboresha huduma za afya kwa kufanya yafuatayo: kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa tiba na dawa; kuimarisha Bodi za afya za Halmashauri, Timu ya Uendeshaji wa Shughuli za Afya ngazi ya Wilaya, kamati za vituo vya afya, zahanati na huduma za

rufaa katika ngazi ya Mkoa, kanda, Hospitali maalum na Taifa; kuboresha huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo; kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza; na kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya (NHIF), Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) na mifuko mingine inayotoa huduma za bima na afya;

(ix) Kuwatambua, kuwasajili na kuwatengamanisha na huduma watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee na watu wenye mahitaji maalum na kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto walio katika mazingira hatarishi;

(x) Kuhamasisha mazoezi na michezo shuleni na katika ngazi ya jamii ili kujenga afya kwa jamii;

(xi) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI takwimu za elimu zilizohuishwa zikijumuisha idadi ya wanafunzi, shule za awali, msingi, sekondari, maafisa elimu kata na shule za bweni ikiwa ni pamoja na shule mpya zinazostahili kupatiwa vibali vya usajili ifikapo tarehe 30 Januari, 2021 ili kuwezesha utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa elimumsingi bila ada;

(xii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya shule pamoja na kuwapatia nyenzo na vifaa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(xiii) Kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, unasihi, ulinzi na usalama wa mtoto, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani;

(xiv) Kujiandaa na kujikinga dhidi ya majanga pamoja na maafa mbalimbali ikiwemo moto, mafuriko na mlipuko wa magonjwa shuleni;

(xv) Kuandaa mikakati ya kushirikisha jamii katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula shuleni;

(xvi) Kuboresha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kuunda na kuimarisha kamati za mazingira katika ngazi za Halmashauri, Kata, Mtaa na Kijiji; kuhifadhi maeneo oevu na vyanzo vya maji; kutunza miti, misitu na maeneo ya hifadhi; kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira; uzoaji na uondoshaji wa taka; na kuendelea kuzingatia kanuni za udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa zuio lililotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mwaka 2019; na

(xvii) Kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114; kuweka mifumo ya mipango miji na matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango kabambe ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kuwa na miji na vijiji vilivyopangika; kutambua na kuweka kumbukumbu za vipande vyote vya ardhi nchini; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika

maeneo ya Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa; na kuweka alama za kudumu za mipaka ya kiutawala ya Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji.

### 1.5. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep

166. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kukamilisha uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep kwa kuzingatia muda uliopangwa pamoja na mambo muhimu yafuatayo:

(i) Usahihi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kuzingatia ukomo wa Bajeti kwa mwaka 2021/22 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2022/23 hadi 2023/24);

(ii) Matumizi sahihi ya namba za miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, mageresho ya kibajeti (GFS codes 2014), vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep na bei za bidhaa kama ilivyoainishwa katika orodha ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA);

(iii) Ukadiriaji sahihi wa stahili za kisheria ikiwemo posho, pango, umeme, simu na maji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Katibu Mkuu (UTUMISHI);

(iv) Takwimu sahihi za Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha ya shughuli zilizopangwa kwenye bajeti; na

(v) Utumiaji wa Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF).

### 1.6. Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

167. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuanzia wiki ya nne ya Februari, 2021. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala mango *(hard copy)* mbili (2) ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi ili kuwezesha kufanyika uchambuzi wa kina kwa ajili ya kuboresha Mpango na Bajeti. Aidha, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwasilisha muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi katika nakala mango. Uchambuzi wa Mpango na Bajeti utazingatia Muundo wa uwasilishaji wa MTEF uliobainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo.

168. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wanatakiwa kuwasilisha nakala mango (*hard copy*) moja (1) na nakala tete (*soft copy*) Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina zilizofanyiwa marekebisho ndani ya siku tano (5) baada ya uchambuzi.

## 1.7. Uwasilishaji wa Randama

169. Maafisa Masuuli wa Mafungu wanaelekezwa kuwasilisha Randama kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya kamati husika itakayotolewa na Ofisi ya Bunge. Uwasilishaji wa Randama uzingatie Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20 na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 kwa kipindi kinachoishia Februari, 2021; Changamoto na utatuzi wake; Maelekezo ya Kamati za Bunge za Kisekta; na Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22.

## 1.8. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

170. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 na miongozo mingine ya iliyopo ya kisekta ya ufuatiliaji na tathmini.

### 1.8.1. Ufuatiliaji na Tathmini

171. Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutenga fedha za ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha kunakuwa na mpango shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

(ii) Kuandaa mpango kazi na mtiririko wa fedha wa utekelezaji wa bajeti kupitia mifumo ya CBMS na PlanRep;

(iii) Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 vinatafsiriwa vema katika Mpango na Bajeti;

(iv) Kujenga uwezo wa watumishi katika vitengo vya ufuatiliaji na tathmini na kuandaa mpango wa kurithisha watumishi wapya maarifa ili kuwa na mfumo wa ufuatiliaji endelevu;

(v) Kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi kupitia mifumo ya kielektroniki (system-based auditing) ili kuongeza ufanisi; na

(vi) Kuhuisha Mipango Mkakati ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuendana na Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Mwaka 2020 hadi 2025.

### 1.8.2. Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

172. Kwa mujibu wa Kifungu Na. 55(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 29(5) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika. Aidha, Taarifa za Utekelezaji za Mwaka ziwasilishwe kabla ya tarehe 15 Oktoba kila mwaka wa fedha. Taarifa za utekelezaji ziandaliwe na kuwasilishwa katika nakala mango na tete kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo. Vilevile, nakala za Taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kadhalika, Maafisa maasuuli watahitajika kuwasilisha nakala tete za taarifa za utekelezaji Ofisi ya Waziri Mkuu.

## SURA YA PILI

## MUUNDO WA UWASILISHAJI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

### 2.1. Utangulizi

173. Sura hii inaainisha muundo, Fomu na mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma katika hatua za uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti.

174. Katika kutekeleza hatua hizo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye nyaraka, mifumo na miongozo ya usimamizi wa bajeti kama ifuatavyo: Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (*CBMS*); Mfumo wa Uandaaji wa Mipango na Utoaji wa Taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma (*PlanRep*); Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na Bajeti (*MTSPBM*); Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 - 2025/26; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (*PIM-OM*); Mfumo wa Malipo na Utoaji wa Taarifa za Matumizi ya Fedha Katika Vituo vya Kutolea Huduma (*FFARS*); Mfumo wa Malipo ya Kielektroniki Serikalini (*GePG*); Mfumo wa Uhasibu Serikalini (*MUSE*); Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (*NPMIS*); Sheria na Kanuni za Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada; na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha Zinazopelekwa Moja kwa Moja kwenye Miradi (*D – Fund Management Information System*).

### 2.2. Maandalizi ya Mpango na Bajeti

175. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 1, 3, 4, 6, 7, 8, 9 na 10 wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti kwa kuzingatia Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF).

(a) **Makadirio ya Mapato**

176. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha makadirio ya mapato kwa kujaza kikamilifu FomuNa. 4 kwa kutumia mageresho ya bajeti (*GFS Codes 2014*) sahihi.

(b) **Makadirio ya Matumizi**

177. Katika uwasilishaji wa makadirio ya matumizi mengineyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza Fomu Na. 3A, 3B na 3C kwa kutumia vizio sahihi vya vipimo na gharama. Aidha, wanaelekezwa kuandaa makadirio ya mishahara kwa kujaza

Fomu Na. 8A-8F na Fomu Na.9 kwa kuzingatia Ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kipindi kinachoishia Juni 2022. Vilevile, katika kupanga makadirio ya matumizi ya maendeleo, Fomu Na. 6 na 6.1 zitatumika na Fomu Na. 10A na 10C zitatumika kupata taarifa muhimu za miradi husika.

178. Katika kupata takwimu za ajira mpya zinazozalishwa kutokana na utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo, Fomu Na. 15A inapaswa kujazwa kikamilifu na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

### 2.3. Utekelezaji wa Bajeti

179. Baada ya bajeti kuidhinishwa na Bunge, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 11A (R), 11A (D), 11B (R), 11B (D), 14B (R), 14B (D) na 14C kupitia mifumo ya CBMS na PlanRep.

### 2.4. Taarifa za Utekelezaji

180. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka kwa kutumia Fomu Na. 12A, 12B, 12C, 13A, 13B, na 13 (C1-C5) na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Fomu Na. 15B inapaswa kujazwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

## MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2021/22 - 2023/24

**Maelezo ya Kisera kwa Ufupi**

i. Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza
ii. Maelezo ya Afisa Masuuli.

**Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo**

1.1 Uchambuzi wa Wadau
1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto
1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

**Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti**

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2019/20
- 2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2018/19
- 2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
- 2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
- 2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2020/21
- 2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2019/20
- 2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
- 2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
- 2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2020/21 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

**Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2021/22 – 2023/24)**

3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (FomuNa.1)
3.2 Fomuya Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (FomuNa. 3A)
3.3 Fomuya Upangaji wa Gharama kwa Kila Shughuli (FomuNa. 3B)
3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (FomuNa. 3C)
3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (FomuNa.4)
3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (FomuNa.6)
3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (FomuNa. 6.1)
3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (FomuNa.7)
3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (FomuNa. 8A)
3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (FomuNa. 8B)
3.11 Kipengele Na.I – Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8C)
3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Wafanyakazi Wasio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8D)
3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu Na. 8E)
3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (FomuNa. 8F)
3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (FomuNa. 9)
3.16 Fomu ya Taarifa za Miradi (FomuNa. 10A)
3.17 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Fungu (Fomu Na. 10C)

## MUUNDO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA ROBO MWAKA

Mada/Ukurasa wa mbele

Yaliyomo

Vifupisho vya maneno

Muhtasari

**SURA YA KWANZA**

Kifungu 1.1 Utangulizi na Hali Halisi

Elezea kwa ufupi majukumu ya taasisi, Lengo la taarifa mbinu na njia zilizotumika

Kifungu 1.2 Vipaumbele/Malengo ya Mwaka

Eleza kwa ujumla Vipaumbele vya Mwaka kama inavyoonekana kwenye MTEF ya Taasisi

**SURA YA PILI: UTEKELEZAJI KWA UJUMLA**

Kifungu 2.1 Hatua Iliyofikiwa

Elezea kwa kifupi utekelezaji na mafanikio ya vipaumbele/malengo ya Mwaka

Kifungu 2.2 Hatua za Kuboresha Utoaji wa Huduma

Elezea mabadiliko yaliyotokea kwenye taasisi yako katika kuboresha utoaji wa huduma

Kifungu 2.3 Changamoto na Mbinu za Kukabiliana na Changamoto

Elezea kwa kifupi Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji kwa ujumla na mbinu zitakazotumika kukabiliana na changamoto hizo.

**SURA YA TATU: HALI YA KIFEDHA**

Kifungu 3.1 Mapitio ya Makusanyo ya Mapato

Eleza mwenendo na mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato malengo ya ukusanyaji, makusanyo halisi na mafanikio au changamoto katika ukusanyaji wa mapato.

Kifungu 3.2 Mapitio ya Jumla ya Utekelezaji wa Matumizi

Eleza hali ya kifedha kwa ujumla kwa kuainisha kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa, fedha zilizotolewa na matumizi

- Kiambatisho Na 1: Fomu Na. 12A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Ufuatiliaji wa Malengo kwa Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati MTEF (CBMS & PlanRep).
- Kiambatisho Na. 2: Fomu Na. 12B: Fomu ya Ujumla ya robo mwaka ya Hatua Muhimu (Vipaumbele)
- Kiambatisho Na. 3: Fomu Na. 13A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka inayotoa Maelezo ya Hali ya Kifedha kwa Ufupi (MUSE).
- Kiambatisho Na. 4: Fomu Na. 13B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina.
- Kiambatisho Na. 5: Fomu Na. 13C1-C5: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kiambatisho Na. 6: Fomu Na. 5: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya mapato kwa Kina.

## MUUNDO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MWAKA MZIMA

Mada/Ukurasa Wa Mbele
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno
Maelezo ya Waziri/ Mkuu wa Mkoa/ Meya/ Mwenyekiti wa Halmashauri/ Mwenyekiti Wa Bodi/ Baraza
Maelezo ya Afisa Masuuli
Muhtasari

**SURA YA KWANZA**

Kifungu 1.1 Utangulizi na Hali Halisi

Elezea kwa ufupi majukumu ya taasisi, lengo la taarifa, mbinu na njia zilizotumika kufikia malengo.

Kifungu 1.2 Dira na Dhima ya Taasisi

Elezea Dira na Dhima ya Taasisi kama ilivyo kwenye Mpango Mkakati

Kifungu 1.3 Malengo ya Taasisi

Elezea malengo ya Taasisi kama yalivyo kwenye Mpango Mkakati/MTEF

Kifungu 1.4 Vipaumbele/Malengo ya Mwaka

Eleza kwa ujumla Vipaumbele vya Mwaka kama inavyoonekana kwenye MTEF ya Taasisi

**SURA YA PILI: UTEKELEZAJI KWA UJUMLA**

Kifungu 2.1 Hatua iliyofikiwa

Elezea kwa kifupi utekelezaji na mafanikio ya vipaumbele/malengo ya Mwaka

Kifungu 2.2 Hatua za kuboresha utoaji wa Huduma

Elezea mabadiliko yaliyotokea kwenye taasisi yako katika kuboresha utoaji wa huduma

Kifungu 2.3 Changamoto na Mbinu za kukabiliana na Changamoto

Elezea kwa kifupi Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji kwa ujumla na mbinu zitakazotumika kukabiliana na changamoto hizo.

**SURA YA TATU: HALI YA KIFEDHA**

Kifungu 3.1 Mapitio ya Makusanyo ya Mapato

Eleza mwenendo na mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato malengo ya ukusanyaji, makusanyo halisi na mafanikio au changamoto katika ukusanyaji wa mapato.

Kifungu 3.2 Mapitio ya Jumla ya Utekelezaji wa Matumizi

Eleza Hali ya kifedha kwa ujumla kwa kuainisha kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa, fedha zilizotolewa na matumizi

**SURA YA NNE: MAPITIO YA RASILIMALI WATU**

Kifungu 4.1 Elezea Muhtasari kuhusu Rasilimali watu iliyopo, nafasi za kazi na masuala mengine ya msingi ikiwemo umri, jinsia, cheo pamoja na uwiano kati ya stahili za mishahara na matumizi mengineyo.

- Kiambatisho Na 1: Fomu Na. 12A: Fomu ya Ujumla ya Mwaka kuhusu Ufuatiliaji wa Malengo kwa Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati MTEF (CBMS & PlanRep).
- Kiambatisho Na. 2: Fomu Na. 12B: Fomu ya Ujumla ya robo mwaka ya Hatua Muhimu (Vipaumbele)
- Kiambatisho Na.3: Fomu Na. 13A: Fomu ya Ujumla ya Mwaka inayotoa Maelezo ya Hali ya Kifedha kwa Ufupi (MUSE).
- Kiambatisho Na. 4: Fomu Na. 13B: Fomu ya Ujumla ya Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina.
- Kiambatisho Na. 5: Fomu Na. 13C1-C5: Fomu ya Ujumla ya Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kiambatisho Na. 6: Fomu Na. 5: Fomuya Ujumla ya Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya mapato kwa Kina.
- Kiambatisho Na. 7: Fomu Na. 13D: Fomu ya Mgawanyo wa Watumishi kwa kuzingatia Cheo (HCMIS)
- Kiambatisho Na. 8: Fomu Na. 13E: Fomu ya Mgawanyo wa Watumishi kwa kuzingatia Jinsia na Umri (HCMIS)

## MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI

Ukurasa wa juu
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno

Utangulizi
Sehemu hii itahusisha maelezo mafupi juu ya Wajibu na majukumu ya kamati katika usimamizi wa bajeti, orodha ya wajumbe kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na orodha ya agenda zilizojadiliwa

1.0 Uendeshaji wa vikao
Sehemu hii itahusisha Ratiba na utaratibu wa uendeshaji wa vikao

2.0 Mapitio ya Muhtasari wa kikao cha kamati kilichopita
Elezea kwa ufupi maazimio ya kikao kilichopita

3.0 Ugawaji wa Rasilimali:
- 3.1 Mgawanyo wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya bajeti kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Kazi
- 3.2 Utaratibu wa ugawaji wa rasilimali kila mwezi kulingana na vipaumbele vya bajeti

4.0 Hitimisho

BUDGET PREPARATION FORMS

## FORM 1: SUMMARY OF ANNUAL AND FORWARD BUDGET ESTIMATES FOR REVENUE, RECURRENT AND DEVELOPMENT EXPENDITURE ('000 SHILLINGS)

**VOTE CODE: …………VOTE NAME: ……………………………………….**

| Description | | | Actual YO-2 | Approved Budget Estimates YO-1 | Annual Budget Estimates YO | Forward Budget Estimates YO+1 | Forward Budget Estimates YO+2 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | | | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** |
| **1. Revenue Estimates** | Government Ceiling/ Grant | | | | | | |
| | Loan | | | | | | |
| | Own Source | | | | | | |
| | Other Sources | | | | | | |
| **TOTAL REVENUE** | | | | | | | |
| **2. Recurrent Expenditure** | PE | PE for Vote proper | | | | | |
| | | PE Subvention | | | | | |
| | | PE Own source | | | | | |
| | Total PE | | | | | | |
| | OC | OC for Vote Proper | | | | | |
| | | OC Subvention | | | | | |
| | | OC Own source | | | | | |
| | Total OC | | | | | | |
| **Total Recurrent Expenditure** | | | | | | | |
| **3. Development Expenditure** | DEV Vote Proper | Govt. Funds | | | | | |
| | | Foreign Funds | | | | | |
| | | Own Source | | | | | |
| | | Other Funds | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | DEV Subvention | Govt. Funds | | | | | |
| | | Foreign Funds | | | | | |
| | | Own Source | | | | | |
| | | Other Funds | | | | | |
| **Total Development Expenditure** | | | | | | | |
| **4. Remittance to Consolidated Fund** | | | | | | | |
| **TOTAL EXPENDITURE** | | | | | | | |

**Note**:
Revenue estimates = All available funds received from various sources
Total Revenue = Total Expenditure
Total Expenditure = Total Recurrent Expenditure + Total Development Expenditure
Total recurrent expenditure = Total PE + Total OC
Total PE = PE for vote proper + PE subvention
Total OC = OC for vote proper + OC subvention
Total Dev= Dev for vote Proper + Dev Subvention
Other Sources = Accrued interest, dividends, interest earned and other returns from investments Other funds = Community contribution, PPP funds from private sector, etc.
Government Ceiling/Grant = Total ceilings or grants received from the Government
Own Source = Revenue collected that form part of institutions spending (MDAs, LGAs and Parastatals)
Loan = Borrowed funds that form part of institutions spending.
Other Sources = Funds received apart from loan, Own Source or Government grants Vote Proper = Revenue collected and expenditure incurred within the same vote Subvention = Government grant through vote proper

$Y_{O-2}$ = Two previous Years (2019/20)
$Y_{O-1}$ = Current Financial Year (2020/21)
$Y_O$ = Budget Year (2021/22)
$Y_{O+1}$ = Forward Budget (2022/23)
$Y_{O+2}$ = Forward Budget (2023/24)

**FORM 3A: MTEF SHEET FOR OBJECTIVES, TARGETS AND ACTIVITY COSTING**

**VOTE CODE: …………VOTE NAME ……………………………………………………………………**

**SUB-VOTE CODE: …………SUB-VOTE NAME……………………………………………………………**

| Objective | Target | Target Type | Activity Code | Segment 2 | Activity Description | Actual YO-2 | Approved Budget Estimates YO-1 | Annual Budget Estimates YO | Forward Budget Estimates YO+1 | Forward Budget Estimates YO +2 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | | | | | | | | | | |
| | 01 | | | | | | | | | |
| | | S | | | | | | | | |
| | | | 01 | A01S01 | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| **TOTAL** | | | | | | | | | | |

$Y_{O-2}$ = Two previous Years (2019/20)
$Y_{O-1}$ = Current Financial Year (2020/21)
$Y_O$ = Budget Year (2021/22)
$Y_{O+1}$ = Forward Budget (2022/23)
$Y_{O+2}$ = Forward Budget (2023/24)

**FORM 3B: ACTIVITY COSTING SHEET**

**VOTE CODE: …………VOTE NAME ……………………………………………………………**
**SUB-VOTE CODE: …………SUB-VOTE NAME ……………………………………………………..**
**OBJECTIVE NO: …………OBJECTIVE DESCRIPTION: ……………………………………............**
**TARGET CODE: …………TARGET DESCRIPTION: ……………………………………..........**

Tick the appropriate (√) ☐ ☐
FYDP III
Other

| Performance Code and Description | GFS Code | Required Inputs | | | Annual Budget Estimates Y0 | | Forward Budget Estimates Y0+1 | | Forward Budget Estimates Y0+2 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | GFS Code Description | Unit of Measure | Unit cost of Inputs | No of Units | Estimates | No of Units | Estimates | No of Units | Estimates |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| TOTAL | | | | | | | | | | |

**Notes**
**Column 1:** Performance Code includes objective, target, target type and activity**;**
**Column 7** equals column 5 x column 6
**Column 9** equals column 5 x column 8
**Column 11** equals column 5 x column 10 YO = Budget Year (2021/22)
YO+1 = Forward Budget (2022/23)
YO+2 = Forward Budget (2023/24)

**FORM 3C: RECURRENT EXPENDITURE SUMMARY OF DRAFT ESTIMATES**

**VOTE CODE: …………VOTE NAME ……………………………………………….**
**SUB-VOTE CODE: …………SUB-VOTE NAME ………………………………………….**

| **GFS Code** | **GFS Code Description** | **Actual Budget** Y0-2 | **Approved Budget Estimates** Y0-1 | **Annual Budget Estimates** Y0 | **Forward Budget Estimates** Y0+1 | **Forward Budget Estimates** Y0+2 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| **TOTAL** | | | | | | |

**<u>Notes</u>**

Columns 5, 6 and 7 is a Summary of Form No. 3(b) Activity Costing Sheet
YO-2 = Previous Years (2019/20)
YO-1 = Current Financial Year (2020/21)
YO = Budget Year (2021/22)
YO+1 = Forward Budget (2022/23)
YO+2 = Forward Budget (2023/24)

**FORM 4: REVENUE ESTIMATES AND PROJECTIONS**

**VOTE CODE: …………VOTE NAME ……………………………………………………………..**
**SUB-VOTE CODE: …………SUB-VOTE NAME ……………………………………………………..**

| **GFS Code** | **Description** | **Actual Collection** Y0-2 | **Approved Estimates** Y0-1 | **Draft Estimates** Y0 | **Forward Budget** Y0+1 | **Forward Budget** Y0+2 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) |
| | | | | | | |
| 14220161 | Miscellaneous Receipts | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | **Total of Sub -Vote** | | | | | |
| | **TOTAL OF VOTE** | | | | | |

**Notes:**
YO-2 = Previous Year (2019/20)
YO-1 = Current Financial Year (2020/21)
YO = Budget Year (2021/22)
YO+1 = Forward Budget (2022/23)
YO+2 = Forward Budget (2023/24)

**FORM 6: DEVELOPMENT EXPENDITURE DETAILS OF ANNUAL AND FORWARD BUDGET**

**VOTE CODE: …………VOTE NAME …………………………………………………………………..**
**SUB-VOTE CODE: …………SUB-VOTE NAME ……………………………………………………........**
**PROJECT CODE: ………………PROJECT NAME: ……………………………………..…...................................**
**OBJECTIVE NO: ………………OBJECTIVE DESCRIPTION: ……....……………………….…………….........**
**TARGET CODE: …………TARGET DESCRIPTION: ………………………………................................**

Tick the appropriate (√)
FYDP ☐
Other ☐

| **Performance Budget Codes** | **Activities Description** | **GFS Code** | **GFS Code Description** | **Annual Budget Estimates Y0** | | | | | | **Forward Budget Estimates Y0+1** | | | **Forward Budget Estimates Y0+2** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Local** | **Foreign** | **L/G** | **D** | **Donor** | **Total** | **Local** | **Foreign** | **Total** | **Local** | **Foreign** | **Total** |
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) | (8) | (9) | (10) | (11) | (12) | (13) | (14) | (15) | (16) |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total of Target | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total of Project | | | | | | | | | | | | | | | |
| **TOTAL OF SUB-VOTE** | | | | | | | | | | | | | | | |

**Notes**
Total Target is Sum of all activities under a Target
Total Project is Sum of all targets under a Project
Total Sub-Vote is Sum of all Projects under the Sub-Vote
Total = Local fund + Foreign fund
L/G = Loan/Grant
D = (Direct to project)

$Y_O$ = Budget Year (2021/22)
$Y_{O+1}$ = Forward Budget (2022/23)
$Y_{O+2}$ = Forward Budget (2023/24)

## FORM 6.1: SUMMARY OF DEVELOPMENT PROJECTS EXPENDITURE ESTIMATES

| Project code | Project Name | Annual Budget Estimates Y0 | | | | | Forward Budget Estimates Y0+1 | | | Forward Budget Estimates Y0+2 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Local | | Foreign | | Total | Local | Foreign | Total | Local | Foreign | Total |
| | | Central Government | Own source | L/G | D | | | | | | | |
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) | (8) | (9) | (10) | (11) | (12) | (13) |
| | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| **Total of Sub Vote** | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | |
| **Total of Vote** | | | | | | | | | | | | |

**Notes**

L/G = Loan/Grant
D = (Direct to project)
YO = Budget Year (2021/22)
YO+1 = Forward Budget (2022/23)
YO+2 = Forward Budget (2023/24)

PBF 4.2

## FORM 7: INSTITUTIONAL RESULTS FRAMEWORK

**VOTE CODE: …………VOTE NAME ……………………………………………………..**

**PROJECTED RESULTS COVERING THE PERIOD FROM FINANCIAL YEAR ………. TO……..**

| Objective Code and Description | Target Code and Description | Indicator Name and description | BASELINE | | INDICATOR TARGET VALUES (AS PER SP) | | | CLASSIFICATION | | | Source of Data / Means of verification |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Baseline Date | Baseline Indicator Value | Y0 | Y+1 | Y+2 | FYDP | SDG | R | |
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

**Notes**

Each row on this form describes a single performance indicator. Indicators are used to measure progress towards achieving objectives; Targets under each objective are assigned indicators for performance measuring. Descriptions of each column are as follows:

**Column1.** Target Code and Description: the target (in words) and its code, being measured by the indicator, for example: ***"Exclusive breastfeeding rate within 6 months increased from 78% to 90%"***

**Column2.** Indicator Name and Descriptions: The indicators name should be in italics while its description (how the indicator is calculated) should be listed below it in a bullet or in parenthesis, for example: *breastfeeding rate as a percentage of children age 6 month"*

**Column3**. Baseline date: describes the most recent date, prior to the current planning phase that the indicator was collected.

**Column4**. Baseline indicator value is the value of the indicator, on the most recent date prior to the current planning phase. If indicator values (and their date) is not known place a dash.

**Columns 5 to 7:** Indicator targets: the expected or projected annual future value of the indicator at the end of the first, second, and third year of implementation, as found in the Strategic Plan. (Y0 = Base Year, (Y+1) = the next financial year, and Y+2 is the next two years and Y+3 is the next three years

**Column 8 to 10**: Place a check mark (tick or X) in the columns FYDP, SDG, and R as follows: FYDP = Five Year Development Plan, SDG= Sustainable Development Goals and R = Ruling Party Manifesto. This will help link the indicator to other coordinating plans

**Column11.** The source is where the indicator data was collected (data source) while means of verification is the supporting evidence.

## FORM 8A: SUMMARY OF PERSONNEL EMOLUMENTS ESTIMATES AT VOTE LEVEL (MDAs/RSs/ LGAs / PUBLIC INSTITUTIONS)

**VOTE CODE: …………VOTE NAME …………………………………………………………..**

| Item | Number of Employees | Basic Salary | Annual Increment | Promotion | Total PE | Employers Contributions | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | ZSSF 13% | PSSSF 15 % | PSSSF 25% (Gratuity) | NHIF 3% | WCF 0.5% | Total Contributions |
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) | (8) | (9) | (10) | (11) | (12) |
| I | | | | | | | | | | | |
| II | | | | | | | | | | | |
| III | | | | | | | | | | | |
| Grand Total | | | | | | | | | | | |

**Notes**
(Summary Items I, II, and III)
**Item I** = Existing Employees on Payroll
**Item II** = Existing Employees not on Payroll
